

Mungu Hamwiti Mtu Hukumuni Bila Ya Kumwonya Kwanza

Jeffersonville, Indiana, USA

Julai 24, 1963

1 “Kuita Malaika elfu kumi,” wakati mmoja angaliangamiza dunia, “bali alikufa kwa ajili yako na mimi.” Hicho ni kitu kama msingi ambao ninataka kuwa na ujumbe wangu kwa ajili ya Jumapili asubuhi, Bwana akipenda, juu ya “Kristo alikuwa nini?” Na sasa tunatarajia labda hawa wasichana wadogo wangeweza kuimba wimbo huo tena kwa ajili yetu, Jumapili asubuhi. Ndugu Wheeler, hakika ninataka kusema ya kwamba kwa kweli una wasichana wawili wadogo wazuri hapo, na kuvaa kwao, na wala hakuna kujipodoa na kadhalika. Waonaonekana kama Wakristo kwangu, nao wanaimba kama wao na kutenda kama wao. Hilo ni zuri sana.

2 Ninaamini nilikuwa nikimwambia mke wangu hivi majuzi, hakika tuna kundi la wanawake walio safi hapa. Ninathamini jambo hilo. Nywele zao ndefu na nyuso zao safi, na wamevaa vizuri. Mimi—mimi—mimi ninapendezewa nanyi kila wakati ni—ninapoingia. Nilimwambia Meda, “Ningetaka kuwapanga wote katika safu wakati mmoja na kuwapiga picha ili kwamba niweze kuyaonesha makanisa mengine jinsi ambavyo kanisa letu lilivyo hapa.” Kwamba hapa tunaposema mambo haya, nao—nao wanatii. Na tunafuraha. Inatufanyia jambo fulani. Tunajua ya kwamba wakati tu—tukiwa na ombi letu, ikiwa mioyo yetu haituhukumu, tunajua ya kwamba Mungu hutusikia.

3 Asubuhi ya leo, rafiki yangu mmoja, aliye mbali sana na hapa, aliandaliwa kwa maziko, wakamkokota na ninii tu, mahututi tu, nilifikiri angelikufa katika dakika chache. Walinipigia simu, ilikuwa ni karibu na mapambazuko. Nikatoka kitandani, nikapiga magoti, nikaanza kumwomba jamaa huyo mzee nami niliweza kwa neema ya Mungu kuwasiliana na roho hiyo, hii hapa ikarudi. Akawa mzima, akarudi tena, mnaona, angali anaishi pamoja nasi usiku wa leo, kwa utukufu wa Mungu. Huyo ni Mzee Ndugu Dauch, mwenye umri wa miaka tisini na moja, akiwa amepita wakati wa safari yake ya maisha kwa muda wa miaka ishirini—ishirini na moja. Lakini Bwana ni mwema na ni mwingi wa rehema, kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

4 Sasa, Ndugu Neville, tunaangaliana mmoja kwa mwingine nami ninajua nina ninii tu kidogo...kama ibada moja zaidi ya kuwa hapa, na hiyo itakuwa ni Jumapili. Wala si—sitaki kumchukua mchungaji wangu, ninapenda tu kumsikia akihubiri.

Jumapili usiku wakati alipohubiri, nawaambieni, nilikwenda hapa pamoja na rafiki yangu kwenye gari hili dogo, kupata sambusa baadaye, Ndugu Evans na Dada Evans, na ndipo tukakutana na Ndugu na Dada Sothmann kule juu. Ndugu Sothmann na hao wengine walikuwa wakizungumza juu ya ule ujumbe mzuri sana. Na, nawaambia, nimeishi kwa huo juma zima, karibu. Na baadhi yao wanasema jinsi ambavyo mbuni anafikiri alikuwa amejificha. Sasa, hiyo ni kweli, hapo anapokiingiza kichwa chake ardhini, bali sehemu kubwa zaidi ya mwili wake ingali imetokeza. Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyofanya wakati mwingine. Tunajaribu kukificha kichwa chetu nyuma ya kitu fulani, daima kuna...labda tungali tunaonekana, mnajua. Yeye huona kila sehemu yetu, mnaona. Kwa hiyo tunathamini sana jambo hilo.

5 Ndipo nikawaza, vema, ninapenda kuzungumza na kanisa na nikawaza, vema, ni—ni ... Ndugu Neville huzungumza na ninyi wakati wote, kwa hiyo basi ninapokuwa hapa chini labda nitakuja huku. Sitaki kuwa mnafiki vya kutosha, na nisitake kupiga simu wala chochote kile, niketi tu huko juu nyumbani na huku kanisa limefunguliwa huku chini. Mimi—sina budi... Ninataka kuwa hapa chini kwa sababu ninawapenda.

Nawaambia, hakika kwa namna fulani mimi ... Hali ya hewa hapa haipatani nami, nami...wala mkoa huu haupatani nami na nina mzio wa hewa iliyo huku. Mara tu hiyo hewa inaponipiga ninapata mabaka ngozini, mwili mzima, mnaona, wala hakuna kitu unachoweza kufanya juu ya jambo hilo. Nami ... Nasi hatujisikii vizuri, hata mmoja wetu, tunapokuwa hapa. Sisi...karibu hakuna mmoja wetu amekuwa akijisikia vizuri sana tangu tumekuwa hapa, maana kwa namna fulani tulikuwa tumeizoea ile hali ya hewa nzuri.

6 Lakini, sasa, kitu kimoja kinachonivutia hapa ni ninyi nyote. Hiyo ni kweli, ninyi nyote. Mnajua, unapata marafiki wengi sana, mimi—mimi ninashukuru sana. Nadhani mimi...kama ningehesabu tu, binafsi, watu niwajuao, huenda wakawa labda ni mamilioni kote ulimwenguni. Wakati mmoja ilikisiwa na mtu fulani, na labda katika kuwajua binafsi, karibu watu milioni kumi. Lakini kuna jambo fulani kuhusu—kuhusu nyumbani, kuhusu watu fulani: Kuna ninii tu ... Kila mtu ana hiyo, kuna watu maalum maishani mwako. Mnajua, ninaamini jambo hilo. Kama hakuna, basi kwa nini mke wetu ni maalum kwetu? Na kwa nini—kwa nini ninii yetu ... Mnaona? Sisi ni ... wake zetu, waume zetu, na kadhalika, ni—ni maalum. Nawe una jambo hilo kwa marafiki. Kuna jambo fulani ama jingine ambalo unataka tu kukutana nao na kuzungumza tu nao. Kuna mambo madogo muhimu.

Nami naweza kuwazia juu ya tindiga hili hapa ambapo kanisa hili dogo lilisimama, na ambapo kabla halijasimama hapa lilikuwa si kitu ila ni di—dimbwi. Hiyo ndiyo sababu barabara ile inakaa mbali kule nje, ipate kulikwepa dimbwi hilo. Hii kwa kweli ni milki, na barabara inapitia karibu sana na mlango pale. Na, ila lilikuwa ni dimbwi. Nami ninakumbuka nikitoka kuja hapa na kujaribu kupata mahali pa kumjengea Bwana kanisa, nami nikiwa ni mvulana mdogo tu.

7 Nami nikawasikiliza hawa, huyu kijana na huyu mwingine hapa, wakiomba muda mfupi uliopita, kwa shauku hiyo yote. Nikawaza, "Mwajua, nilikuwa nikiweza kuomba namna hiyo, bila ya kupumua, karibu sipumui." Kisha unazeeka zaidi, kwa namna fulani unapunguza mwendo kidogo, mwajua, na hivyo. Ungali unapiga hatua, bali uko "kwenye gia ya pili" kama nilivyomwambia Ndugu Woods pale nje. Lakini, halafu mradi tu ... Na halafu baada ya kitambo kidogo, unaingiza gia ya chini, unapofikia kwenye sabini ama themanini, nadhani. Lakini, mwajua, ninii...ungali unapiga hatua, haidhuru. Mradi tu unaweza kusogea, inaleta tofauti gani? Muda kidogo tu zaidi kufika kule.

8 Ninakumbuka jinsi nilivyokuwa nikiomba, na papa hapa katika magugu haya, papa hapa ambapo mimbara hii inasimama sasa, karibu tu na mahali ilipo, hapo ndipo nilipopigilia kigingi kidogo ambapo nilitaka kuiweka mimbara. Bwana Mungu anipe mahali hapa. Naam, bwana. Sasa, pale pale penye jiwe la pembeni pana ushuhuda wangu wa ono asubuhi ile nilipoliweka, wakati ilikuwa ni vigumu kwangu kuwazia basi, kasema, "Hii siyo maskani yako, bali fanya kazi ya mwinjilisti," Yeye akasema. Niliangalia huko nje nikauona ulimwengu wote pale, na mbingu angavu za bluu, na watu wakija toka kila mahali; uko kwenye lile jiwe la pembeni pale. Jinsi sikujua kabisa kwamba hilo lingetukia, hata ingawa ono lilisema hivyo; bali halishindwi, litatukia hapo haidhuru.

9 Nimekuwa kwenye mahojiano mengi sana juma hili, kwa sababu, Jumapili, Uwepo wa neema wa Bwana ulishuka chini. Nami nilitarajiwa kuondoka Jumatatu.

Nime...hatujachukua likizo bado, watoto. Likizo yangu inakuja baadaye, baadaye kidogo. Lakini ninataka kuwachukua watoto kwa muda kidogo. Inawabidi kurudi na waende shuleni sasa, na kwa hiyo niliwazia juma hili lingekuwa ni wakati unaofaa. Ninaelekea Chicogo juma lijalo kwenye ule mkutano kule.

Lakini basi u—upako wa Roho, niliwazia, "Huu ndio wakati wa kufanya mazungumzo ya faragha." Huu ndio wakati ambao haya...ambapo ninaweza kuendelea na baadhi yao kule. Na kuna ... Ninawaona baadhi ya watu wameketi hapa waliokuwa mle chumbani. Wanajua kama Bwana alikutana nasi ama la.

10 Jambo la ajabu ambalo...kila mmoja mbali na wanawake fulani ambao Billy aliwaingiza muda kidogo tu kabla, mama mmoja kutoka Louisville, alikuwa na msichana mdogo aliyekuwa hapa, nafikiri hasa ni wafuasi wa Church of God huko Louisville, ama kitu kama hicho. Lakini kila kisa, kila mmoja wao aliyeingia, kabla sijaondoka nyumbani Roho Mtakatifu aliniambia ni nani angekuwa hapa, yale wangeuliza. Nami nikaandika kwenye kipande cha karatasi na kusema yale hasa wangeuliza na maswali yao jinsi wangeyauliza, na jinsi wangejibiwa. Ndipo ningewaambia, ningesema, "Hivi ndivyo tu wewe...angalieni sasa, dakika chache zilizopita hapa, yale Roho Mtakatifu..." Nyosha mkono wako kwenye dawati na useme, "Unaona? Yeye aliniambia hili kabla hujaja." Mnaona? Lakini wakati nilipokuwa huko nyumbani, ni nani angekuwa pale na jinsi mambo yangekuwa, jinsi mtazamo wao ungekuwa, na yote kuhusu jambo hilo, kabla hata sijaondoka nyumbani.

11 Niliona wakati, mara nyingi, wakati ningekuwa nikishuka kuja barabarani, nikiomba, ningeuona huo mstari wa maombi mbele zangu na kujua kila jina ambalo lingekuwa kwenye mstari wa maombi, kabla sijapata kufika hapa. Hiyo ni kweli. Na hata kujua mahali walipokuwa wameketi kanisani na kile wangeninii...jinsi wangukuwa wamevaa na vile wangeonekana. Huwaambii watu kila kitu namna hiyo. Ninayi ... Yapo mambo yanayotendeka ambayo kamwe huwaambii. Si lazima kuwaambia. Ninawaambia tu watu mambo ninayoona yatawasaidia, wakati Bwana anaponisukuma kuwaambia, aseme, "Sema jambo hili." Usingetaka kusema kila kitu ambacho umeona, kwa sababu hilo lisingekuwa ni sawa, mnaona, unaninii tu...bila shaka, unaingia katika shida na kila kitu namna hiyo. Huna budi kujua jinsi ya kushughulikia mambo hayo kwa Roho wa Bwana.

12 Nimekuwa na watu waliosimama mbele zangu na kuniuliza maswali, ninajua kabisa, bali nisingewaambia, kwa sababu nilijisikia tu kuzuiwa nisifanye hivyo. Mnakumbuka, ninaamini ilikuwa ni Jumatano iliyopita usiku, nilihubiri juu ya, *Mfungwa*. Mnaona? Mnaona, unataka kumwambia mtu huyo, bali kitu Fulani kinasema, "Usifanye hivyo." Roho anasema, "Usifanye hivyo. Usifanye hivyo." Hata hivyo karama inakiangalia moja kwa moja, mnaona. "Usifanye hivyo. Usifanye hivyo." Mnaona, kwa hiyo afadhali usimwambie; hapo utaingia kwenye shida na Mungu.

13 Sasa, hatuji hapa chini usiku wa leo kusimama tu hapa. Tunataka kusikia Neno la Bwana. Mmekuwa mkiomba nasi tumekuwa na wakati mzuri sana, na—nami...daima ninaposhuka kuja huku ninajua ninaleta tu kitabu kidogo chenye mihtasari maana kuna... Wakati mwingine Ndugu Neville ni mnyofu sana yeye anaendelea tu kuniuliza, "Je! utafanya hivi," ama "ufanye vile," ama "kuhubiri?" Nami ninapitisha macho hapa mpaka ninapata fungu la namna fulani na ndipo tutalianzia hapo. Nami nina hakika ... Sasa, hakikisheni Jumapili ...

Sasa, mimi si ... Kamwe hatujui, hatuwezi kujua. Mnaona, nimekuja hapa nyakati zingine na—na somo moyoni mwangu ambalo nilitaka kulizungumzia, ndipo ninafika hapa na kulibadilisha kabisa. Nami nimekuwa na Maandiko yaliyoandikwa, ninasema, "Nitatumia fungu hili, nitatumia Maandiko haya. Yanaposhuka, nitasema *hili, lile* ama *linginelo*." Nitayaandika, kama vile tu, Wakorintho wa Kwanza 5:15, na Wakorintho wa Pili 7:1, na Mathayo 28:16, kadhalika, ninayaingiza ndani tu jinsi hiyo, hapa chini namna hii, na

kuyaandika hayo Maandiko. Nami ninaangalia pale chini, ninajua yale Maandiko yanayosema pale; wakati mwingine hata nisyaguse hayo, ninapitia njia nyingine kabisa, kwa jumla. Wala kamwe hatujui.

14 Kwa hiyo sasa, Bwana akipenda, ninataka kuzungumza, katika kumaliza milolongo hii midogo ya ibada tangu tuwe hapa, Jumapili asubuhi, juu ya jambo muhimu sana. Kwa hiyo, sasa, njoni mapema, mkiwa tayari kuchelewa zaidi kidogo tu, labda mnamo saa nane, kitu kama hicho. Na kwa hiyo ni ... Nina karibu Maandiko thelathini ama arobaini yaliyoandikwa hapa tayari juu ya somo hili, bali nafikiri kile ninii...kile nitakachojaribu kufanya, endapo Roho Mtakatifu atanisaidia, kuushika Ujumbe na mahali ulipo sasa, na kuujengea papo hapo mahali ulipoanzia, na kuujenga kuufikisha wakati wa sasa.

15 Ili kwamba wakati ni—nitakapoondoka kuelekea Chicago, basi nitaenda moja kwa moja hadi Arizona, halafu niendeleo mbele, zaidi na zaidi. Na huenda ikawa, kadiri nijuavyo mimi, huenda ikawa ni mwaka ujao tena, labda msimu ujao wa kiangazi, kabla sijarudi tena maskanini, isipokuwa iwe ni kupitia hapa tu tena, maana nina mikutano.

Na Billy, sasa hivi, anaandaa ya nchi za ng'ambo kwa ajili ya ziara ya ulimwenguni kote kuanzia mara baada ya Krismasi. Nami sina nafasi tena mpaka karibu kwenye Desemba, na, vema, labda juma la kwanza la Desemba, Dallas. Kwa hiyo basi—basi Januari tunataka kuanza ziara ya kote ulimwenguni, kuuzunguka wote, kabisa, nasi tunaiandaa hiyo sasa, tukitaka kujua mahali Bwana atakapoongoza. Na—nami—ninashukuru sana kwa ninii...hata kwa watu, wahudumu, kadiri ninavyonena dhidi ya madhehebu ya —yao na mambo kama hayo.

16 Mnajua, kwenye vitabu vilivyo moja kwa moja kule nyuma sasa, Ndugu Roy Borders hushughulikia mialiko, na tangu Krismasi, mwanzoni mwa mwaka, kumekuwako na zaidi ya mialiko elfu moja kote ulimwenguni. Mialiko elfu moja imekuja kule nyuma. Kwa hiyo Bwana hana budi kuniongoza tu kwamba niende kwenye upi kati ya hiyo, na la kufanya. Tunamtegemea tu. Usingeweza kuichukua yote. U—usingeweza kuchukua zaidi ya minane ama kumi katika msimu wa kiangazi hata ufanye nini, katika—katika ninii nzima...isipokuwa iwe uende tu usiku mmoja hapa na usiku mwingine pale, na hiyo ni...wanaomba wapewe majuma mawili ama matatu, na kadhalika, kadiri unavyoweza kukaa, ama baadhi yao wanasema "muda wowote tu Bwana atakaokuongoza," na—na yote namna hiyo, kwa hiyo kamwe hujui uanzie wapi ama ufanye nini. Kwa hiyo tunayaweka tu pale mbele za Bwana, tukisema, "Sasa, Wewe twambie, Baba wa Mbinguni." Nanyi mnisaidie kuombea jambo hili, mnaona, mnisaidie kuomba ya kwamba tunaweza kumaliza jambo hili.

17 Nami niliwazia, baada ya kuwa na ibada ya uponyaji Jumapili iliyopita, halafu labda Jumapili hii kama tukichukua tu mafundisho na kuyaleta moja kwa moja na kuonesha ni—ni wakati gani tunaonini...mahali tulipo, kusudi lenye sehemu tatu la mpango mkuu wa Mungu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu ni—ni—ni—ni—ni lipi, na kulishusha hadi leo, lile kusudi lenye sehemu tatu la mpango wa Mungu, ule mpango. Ninashughulikia sehemu ya pili sasa, kuyachukua Maandiko, kuyatafuta na kuyaweka mahali pake.

Sasa, hebu tuone, hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi.

18 Bwana Yesu, Mchungaji mkuu wa zizi la kondoo, tumekusanyika hapa usiku wa leo katika Jina Lako lenye neema, takatifu. Tunakupenda, Bwana, na tunakushukuru kwa ajili ya usiku huu wa mkutano wa maombi, kwa ajili ya nyimbo za kanisa kwa kuwa tumeziimba kwa furaha mioyoni mwetu, na—na tukawasikia walipokuwa wakiingia, wakipiga makofi. Na ndipo tukapiga magoti yetu na sote tukaimwaga mioyo yetu Kwako, na kukushukuru Wewe kwa yale umetufanyia, na—na kukuomba uendeleo kutembea pamoja nasi.

Na sasa saa imewadia ya kusomwa kwa Neno na jambo fulani la kuzungumzia, kwa watu. Tuelekeze katika mawazo yetu, Baba, na upate utukufu. Na useme jambo fulani usiku wa leo, kupitia kwetu, litakalotusaidia sisi sote kutoka hapa na kusudi moja mioyoni mwetu kuishi vizuri zaidi na karibu na Wewe kuliko tulivyowahi kufanya. Hilo ndilo lililotuleta hapa, Bwana, tupo hapa kujua mengi zaidi kukuhusu Wewe. Nasi tunaomba ya kwamba utaufunua Utu Wako mkuu kwetu usiku wa leo katika ufunuo wa Neno Lako, kusudi tupate kujua jinsi ya kuwa M—Mkristo bora na jinsi ya kufanya katika siku hizi za mwisho. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

19 Sasa, macho yangu yanaangukia somo hapa la Isaya, Isaya 38. Hebu na tusome Isaya, Isaya 38.

Siku hizo Hezekia aliugua akawa katika hatari ya kufa; na Isaya nabii, mwana wa Amози, akaenda kwa mfalme, akamwambia, BWANA asema hivi, Tengeneza mambo ya nyumba yako; maana utakufa, wala hutapona.

Basi Hezekia akajigeuza, akaelekeza uso wake ukutani, akamwomba BWANA.

Akasema, Ee BWANA, kumbuka haya, nakusihii, kwamba nimekwenda mbele zako katika kweli na kwa moyo mkamilifu, na kutenda yaliyo mema machoni pako. Na Heze- ... Hezekia akalia sana sana.

Ikawa neno la BWANA likamjia Isaya, kusema,

Enenda ukamwambie Hezekia, BWANA Mungu wa Daudi, baba yako, asema hivi, Mimi nimeyasikia maombi yako, nimeyaona machozi yako; tazama, nitaziongeza siku zako, kiasi cha miaka kumi na mitano.

20 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye usomaji huu. Ni somo bora sana kwa ujumbe mfupi hapa, ninaamini. Ninataka kuuita: *Mungu Hamwiti Mtu Hukumuni Bila Ya Kumwonya Kwanza*. Nasi ina—ina—inatupasa kushika m—msingi ama jukwaa lake hapa, katika somo hili usiku wa leo, Mungu akimwonya mtu kabla hajamleta kwenye kifo chake.

Sasa, kila mtu ana hili. Huenda tukasema, “Vema, jamaa *huyu* alikufa bila ya onyo.” La, la, la. Mungu kamwe ... Hujui ni nini kilichokuwa kwenye moyo wa mtu huyo, hujui yale yamekuwa yakiendelea katika maisha yake. Mnaona? Mungu kamwe hamleti mtu yeyote kwenye kifo chake bila ya kumwonya kwanza kuhusu hilo, akimwambia, ni jambo fulani, matayarisho. Mungu ni—ni mwenyezi, na Yeye—Yeye hubisha kwenye moyo wa kila mtu, akimpa nafasi ya kuja. Sasa, anaweza kumwonya mtu naye akakataa, na—na kumtikisia kichwa chake na kwenda zake, aseme, “Aha, ni hisi tu ya ajabu-ajabu, itaniondoka.” Lakini, hata hivyo, ilikuwa ni Mungu, Mungu akinena naye.

21 Na Mungu kamwe haleti hukumu juu ya nchi bila ya kuwaonya watu kwanza. Mungu hatendi neno bila kwanza kutangaza atakalofanya. Naye huwapa watu chaguo, nawe unaweza—unaweza kutenda lililo jema ama baya. Hiyo ni ninii Yake ... Mnaona, Mungu kamwe hawezi kubadilisha ta—tabia Yake. Mpango Wake kamwe hauwezi kubadilika kutoka kwa ule alioanza nao, kwa kuwa Yeye hana kikomo na mpango Wake pamoja na mawazo Yake yote ni makamilifu. Kwa hiyo, kama angeubadilisha, hiyo ingeonesha ya kwamba Yeye alikuwa amejifunza zaidi. Kwa hiyo, kwa kuwa hana kikomo, Yeye hawezi kujifunza zaidi. Uamuzi Wake—Wake—Wake wa kwanza daima ni mkamilifu, wala hakuna kitu kinachoweza kuubadilisha kamwe. Mnaona?

Mungu, kabla ya mwanadamu kuwekwa...hajapata nafasi ya kutenda mabaya, Mungu alimweka kwenye msingi ambapo angeweza kukubali ama kukataa, angeweza kupokea ama—ama asipokee.

22 Aisee, jambo lingine, kama yule mhudumu humu ndani, Ndugu Baker, ninaamini alikuwa kwenye ma—mazungumzo ya faragha hivi majuzi, ninayo maswali yake ambayo alikuwa ameniandikia juu ya uzao wa nyoka. Ninayo yamewekwa hapa nyuma sasa. Endapo yupo hapa, mbona, vema... Simwoni mahali popote wakati huu. Lakini liko hapa. Yeye na mkewe, mtu mzuri sana na mwa—mwanamke, bali wa—wasingeelewa mambo machache kuhusu mafundisho ya uzao wa nyoka, jinsi ambavyo—ambavyo...baadhi ya maswali fulani kuhusu yale niliyokuwa nimesema, na—na mahubiri zaidi ya hilo, na—na kunena kuhusu kule—kule kutiwa mimba na kadhalika. Lakini mimi...basi ni kama tu yule ndugu, mtu mzuri, Mkristo tu kwa miaka kadhaa ama miwili, bali ni kuwa hakuelewa, mnaona.

23 Ni vigumu kama huna ... Inakubidi kumtegemea Roho Mtakatifu kwa sababu Biblia hii imeandikwa katika mafumbo. Huwezi tu kuketi chini na kuisoma kama gazeti. Imefichwa. Naam, bwana. Ungewezaje kamwe kumhesabia Mungu haki wakati alipomwambia Musa kule juu, kasema, “Sasa, msifanye sanamu zozote za kuchonga,” katika amri zake, “msifanye chochote mfano wa Mbinguni, Malaika ye—yeyote, wala chochote kile, msifanye sanamu zozote za kuchonga,” na hata hivyo siku hiyo hiyo akamwambia afinyange Malaika wawili kwa shaba na kuwaweka papo hapo kwenye kiti cha rehema, mahali ilipo neema? Mnaona? Huna budi kumjua Mungu na Tabia Yake kabla hujalielewa Neno Lake. Yeye—Yeye—Yeye ana ufunguo wa Neno hilo, Mwenyewe, na Yeye—Yeye ndiye tu anayeweza—anayeweza kulishughulikia na kulifungua, na kwa hiyo Yeye ndiye anayepaswa kulifunua.

24 Na sasa, tunaona ya kwamba Tabia Yake ilikuwa, hapa, daima kumwonya mtu kabla ya hukumu, kulionya taifa kabla ya hukumu, na kadhalika. Yeye daima hutoa onyo Lake, ukumbusho kwetu, wa wajibu. Sisi tunawajibika, na Mungu ametuweka hapa duniani kwa sababu fulani, na sababu hiyo ambayo kwa hiyo Yeye ametuweka hapa, sisi tunawajibika Kwake kwa sababu hiyo. Unapaswa kwenda Kwake na uone kile anachotaka ufanye. Mnaona? Usiponinii...

Kama ulienda kumfanyia mtu kazi, naye akakupa kazi kwenye ranchi, ama kitu kama hicho, nawe ulienda tu kwenye ghala la shambani na ukaketi tu pale, na useme, “Vema?” Mnaona, huna budi kwenda kumwuliza yale anayotaka ufanye, kisheru ufanye. Kama unamfanyia mtu fulani kazi, tafuta kujua wajibu wako ni nini.

Na basi kama maisha yetu yapo hapa du—duniani, basi inatupasa kumwendea Yeye aliyetuweka hapa, na, “Bwana, ungetaka nifanye nini? Nini—nini—nini nifanye? Kwa nini nipo hapa?” Kama ni kuwa mke nyumbani, mwosha vyombo, kama ni kuwa... Lolote ambalo Mungu anakutaka ufanye, basi lifanye hilo vizuri kabisa unavyojua kulifanya. Haidhuru ni dogo jinsi gani, haidhuru ni dogo jinsi gani, huna budi kulifanya.

Unasema, “Vema ...” Shida yake, ni, kila mmoja wetu anataka kufanya kazi ya mtu mwingine. Sote

tunataka kuuchukua mpira, kama tusemavyo, mnaona.

25 Kama saa hii hapa, sasa, kila msogeo mdogo humo ndani una mahali pake. Sasa, kila sehemu yake haiwezi kuwa ni mikono. Sasa, ninaangalia tu mikono kuona ni saa ngapi. Lakini kama moja ya magurudumu mle ndani likienda kombo, hiyo haitaweka muda sahihi.

Na hivyo ndivyo ilivyo kwa watu. Sote tumeninii, Mwili wa Kristo, hatuna budi kuwa katika mahali petu, katika upatano. Mnaona? Na ndipo tunaweza kuangalia kote na kuona ni saa ngapi. Mnaona? Ndipo ulimwengu unaangalia kuona ni kitu gani. Mnaona? Mnaona? Lakini wanakuangalia. Na kama wewe ni springi dogo tu, springi kuu, ama chochote ulicho, wewe fanya kazi vizuri sana uwezavyo kufanya.

26 Sasa, kwa sababu, tuna jukumu ambalo hatuna budi kujibu kwa Mungu siku moja. Kila mtu anayekuja juu ya uso wa nchi hana budi kujibu kwa Mungu kwa ajili ya wajibu fulani. Na, kwa wengi wetu, usimamizi, itatubidi kujibu. Sisi ... Wajibu ni uwakili tuliopewa na Mungu, sijali ni jambo gani. Kama nilivyosema dakika chache zilizopita, "mke wa nyumbani," basi uwe mke wa nyumbani halisi. Hiyo ni kweli. Kama ni kuwa mkulima, uwe mkulima halisi. Chochote kile ambacho Mungu amekuweka kufanya, una utumishi kwa jambo hilo, huna budi kuwajibika kwa hilo kwa Mungu, kwa kuwa inahitaji vitu hivi vyote kufanya jambo hilo.

27 Hezekia aliambiwa atengeneze mambo na awe tayari kwa sababu kwamba ilimbidi kukutana na Muumba wake. Sasa, Hezekia alikuwa ni mfalme, na m—mtu mashuhuri. Je! Mliona ombi lake hapa? "Bwana, nakusihi unihurumie. Ni—nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu." Ni ushuhuda wa jinsi gani kwe—kwe—kwetu leo, na unapaswa kuwa, mtu anayetembea mbele za Mungu.

Hata kifo kilitamkwa juu ya mtu huyo na hata hivyo Mungu akabadilisha nia Yake kumhusu yeye, kwa maana Hezekia alitaka kufanya jambo fulani na Mungu alisema Yeye "atatupa shauku za moyo wetu." Na wakati wa Hezekia ulikuwa umewadia, naye—naye akaugua kansa, ama kitu kama hicho, na—nao waliuita "jipu" siku hizo, bali tunajua majipu kwa kawaida hayakuui, yanapona tu. Lakini labda ilikuwa ni kansa, nayo ilijifungua kama jipu. Ndipo—ndipo Mungu akamwambia Isaya, kasema, "Panda uende kule ukamwambie ya kwamba atakufa." Naye Hezekia alikuwa na kitu alichotaka kufanya bado. Alikuwa—alikuwa ...

28 Unapomsihi Mungu kwa kitu chochote, huna budi kuwa na sababu yake. Ni kama tu Andiko hili ninalorejea kwake mara nyingi sana, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitie shaka, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako." Sasa, hilo kwa jumla linategemea lengo na kusudi, mnaona, la sivyo halitatukia. Mnaona?

Huwezi tu kutoka uende hapa nje... Hapo ndipo wengi wetu wanapofanya makosa mengi, ni kutoka kwenda na kusema, "Sasa, nitakuonyesha nina imani ya kufanya jambo hili." Sasa, kwanza kabisa, umekosea. Mungu hakupi karama ili tu uzichezee.

Kama nilivyokuwa nikisema muda mfupi uliopita, Yeye hakuonyeshi maono upate tu kuyachezea. Hayo si ya kuchezeza. Hayo ni matakatifu. Yatumie tu katika...kama Bwana atakavyokuruhusu. Kuwa mfungwa Kwake. Haidhuru ni kiasi gani unataka kumwambia jamaa huyo kwamba amekosea, na vile hili, lile, ama linginelo, wewe tulia mpaka Mungu atakaposema hivyo. Mungu atakaposema hivyo, basi unaweza kuja na BWANA ASEMA HIVI! Mpaka hapo, sahu tu jambo hilo.

29 U—ulimwengu siku hizi ni kama vile tu Hezekia alivyokuwa wakati huo, umeonywa. Daima unaendelea kuonywa. Kanisa linaonywa. Na, sasa, mambo haya hayatukii tu kwa—kwa bahati. Wote wana kitu fulani nyuma yao.

Sasa, Hezekia, akiwa ni mgonjwa, akiwa na jipu hili, haikuwa ni kwa bahati. Mungu alimtuma Isaya huko juu na akamwambia atengeneze mambo ya nyumba yake sasa kwa sababu atakufa. Ndipo Hezekia akalia, na kumwambia Mungu, "Nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu nami na—nakuomba uyaokoe maisha yangu kwa jambo fulani, jambo zuri, jambo la Mungu."

Mungu alimwambia nabii, akasema, "Rudi ukamwambie."

30 Sasa hilo si ni la ajabu? Hezekia alikuwa ndiye mtu mkuu kuliko wote nchini. Mnaona? Hezekia alikuwa ni mfalme, na mtu mcha Mungu. Yeye alikuwa ni mtu halisi, kama angeweza kumsihi Mungu kwa jambo hilo wala Mungu hakumkemea kwa hilo, "Nimetembea mbele zako kwa moyo mkamilifu." Sasa hilo linasema mengi sana. Mnaona?

Mungu kamwe hakusema, "La, Hezekia, hukufanya hivyo," bali alikiri ya kwamba alifanya hivyo. Naye akasema, "Nita—nitayaokoa maisha yako kwa muda kidogo zaidi." Mnaona? "Nitakupa ombi lako," mnaona, kwa sababu alikuwa ni mtu mwenye haki, alikuwa m—mtumishi halisi wa Kristo.

31 Na ndipo tunajisikia ya kwamba tuna haki ya kuomba jambo fulani kama—kama lengo letu ni sawa, halafu nia yetu kwake.

Sasa, tunaona siku hizi ya kwamba kwa miaka mingi iliyopita, ningesema kwa miaka kumi na mitano, hata na zaidi, ya kwamba daima kumekuwako na onyo kote nchini, "Tubuni, la sivyo mtaangamia!"

Mnaona, nilikuwa nikizungumza leo na mke wangu mapema asubuhi hii tu, nami...mapema kwenye kiamshakinywa, tulikuwa tumeketi mezani tukizungumza kabla sijaondoka. Nami nikasema, "Mke wangu ..." Alikuwa akizungumza juu ya Billy Graham, na kuhusu mke wake, jinsi ambavyo wanajaribu kuishi maisha ya kawaida tu na kadhalika. Nikasema, "Huyo ni mtumishi halisi wakati anapojaribu kuto-...wakati yeye... mtu labda anapata milioni mbili ama tatu kwa mwaka katika miamsho yake, bali hazipokei, taasisi yake huzichukua, inazirudisha kazini na matangazo, na kadhalika. Naye Billy hupata kama elfu ishirini na tano kwa mwaka."

Akasema, "Angewezaje kutumia ishirini na tano elfu kwa mwaka?"

Nikasema, "Hu—huchukua zile tu zinazompasa kuchukua, hivyo tu. Yeye ana nyumba ya kulipia, na kila kitu." Nikaendelea, nikasema, "Ninamheshimu sana Billy Graham," nikasema, "kwa sababu yeye ana ujumbe, na ujumbe huo ni toba."

Halafu, nawaambia, hakuna mtu nimjuaye, aliye nchini siku hizi, ambaye Mungu amemtumia kwa ujumbe huo kama Billy Graham. Loo, amehubiri bila kusita, naye husimama hapo tu na, ninamaanisha, yeye anawaita hao wanasiasa na wafuasi wa kanisa wakatubu. Lakini huo ndio umbali anaoenda.

32 Na huyu hapa Ndugu Oral Roberts anakuja, mtumishi mwingine mashuhuri wa Bwana. Wala hakuna mtu anayetoka nje huko na kujilinganisha na Oral Roberts. Ule mshiko wa nguvu nyingi mno wa ku—kuwatoa tu pepo wachafu na kuliitia Jina la Bwana na—na mihemko midogo-midogo, na kadhalika, kuhusu uponyaji wa Kiungu. Hiyo ni kweli kabisa. Huyo hapo mjumbe kwa Wapentekoste.

Huyo hapo mjumbe kwa ulimwengu wa kanisa la kimadhehebu, mnaona, na ulimwengu baridi.

Halafu angalia huku kwenye huduma yetu ndogo nyeyekevu, ikisimama "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," mnaona. Hiyo inafanya nini? Inaliita kundi hilo la Bibi-arusi, mnaona. Mnaona? Mnaona, ina—inaita kutoka kwenye makundi hayo yote mawili. Ni kutoa Gurudumu kutoka kwenye gurudumu. Mnaona kile ninachomaanisha?

33 Na kisha Mungu anauthibitisha ujumbe huo ambao Billy Graham anahubiri. Mungu huwaponya wagonjwa kwa maombi ya Oral Roberts. Na Mungu huzaa mambo ambayo Yesu ... anathibitisha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na ni kuyaita mambo hayo ambayo ... Ni jumbe za wakati huu. Na kila mmoja wa jumbe hizo unaita, "Tubuni, la sivyo mtaangamia!" Hiyo ni kweli. "Tubuni, la sivyo mtaangamia!" Hakuna matumaini, yote yamekwisha. Ulimwengu umeonywa juu ya Kuja Kwake. Kila mmoja wa jumbe hizo unanena na kuonya juu ya Kuja kwa Bwana Yesu, kwa kanisa la kimadhehebu ...

34 Kumbukeni, Mungu daima yuko katika tatu-tatu. Kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuhesabiwa haki, na ubati-...na kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; kadhalika; Yeye yuko katika tatu-tatu.

Sasa, Mungu ndiye huo ujumbe wa toba kwa kanisa la kawaida. Mungu yuko katika ujumbe huo wa uponyaji wa Kiungu kwa kanisa la Kipentekoste. Mungu yuko katika Ujumbe kwa Bibi-arusi. Mnaona? Kwa hiyo tunaona ya kwamba wote wanaita, mmoja kwa *huyu*, *huyu* kwa *yule*, na *yule* kwa *yule*. Mungu akiliita kanisa kutoka ulimwenguni; ninii...akiliita kanisa katika kanisa la kimadhehebu liingie katika Pentekoste; na kumwita Bibi-arusi kutoka katika Pentekoste. Mnaona?

Kama vile Luther, Wesley, na sasa. Mnaona, yote yameonyeshwa kwa mfano wala hakuna kosa kwake. Nimegusia kwenye miisho yake yote, na kando yake, na ndani na nje yake, na kulionyesha kwa Maandiko, utaratibu wake wa miaka, mpaka tunajua ya kwamba ni Ukweli mtupu. Mnaona? Hakuna kosa. Jumapili natumaini ya kwamba Mungu atalididimiza ndani sana hivi kwamba kamwe hamtaweza kuachana nalo. Mnaona?

35 Sasa, Mungu akitoa onyo, "Jiandaeni kwa ajili ya hukumu." Yale mabomu ya atomiki yako kwenye mabanda yake, kila kitu kiko tayari. Na Mungu, kabla hajaliruhusu jambo hili litukie, anatoa wito kotekote, kama alivyofanya Sodoma, "Tokeni kwake. Iweni tayari. Kuna jambo fulani litakalotukia."

Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kabla Mungu hajatuma maji kuuangamiza ulimwengu katika ule ulimwengu uliotangulia ile gharika uliokuwa umetokomea katika dhambi, kama vile Yesu alivyosema waziwazi ya kwamba ilikuwa ni siku kama hii kabisa. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Jinsi ambavyo wanawake watakuwa wamepotoka, na—na kuo na kuolewa, na—na ufanisi mkuu wa sayansi, na walio werevu na wenye elimu wakiingia upande wa kiakili, nalo Kundi dogo nyenyekevu limeketi upande mmoja wakiingojea hukumu ijayo na kuiepuka. Na kabla Mungu hajatuma hukumu hiyo, Yeye alituma nabii.

Kama tu vile alivyomfanyia Hezekia, Yeye alisema, "Tengeneza mambo, kwa kuwa hukumu iko tayari kuanguka."

Naye akawafanya watu wawe tayari kwa ajili ya wakati huo. Nuhu aliwatayarisha watu, nao ulikuwa ni wito wa rehema kabla ya hukumu.

36 Ninawi ulijulishwa kabla ya wakati wao. Mungu aliangalia chini kuelekea Ninawi, na akasema, "Ni—nimechoshwa na kukasirishwa na mambo haya." Na—na—nafahamu ya kwamba—ya kwamba ... ingawa ulimwengu huo mkuu, wa kipagani, wa Mataifa ... Jiji lao, kama ilivyokuwa katika siku hizo, waliwapima kwa mji; sasa ni kwa mataifa, sasa baada ya idadi ya watu kuenea jinsi imeenea. Yeye alisema, "Jiji hilo kubwa limezama, kwa jumla, katika dhambi."

Na Mungu, kabla hajatoa hukumu, Yeye alituma ujumbe wa onyo, "Tokeni kwake! Jiwekeni sawa!" Angalieni, nabii hakusema kitu ila—ila kuninii... Kasema, "Katika muda wa siku arobaini mji huu utaangamizwa."

37 Na, loo, jinsi ambavyo wakati mwingine ni vigumu kufanya mambo kama hayo, kuwaambia watu. Kama nabii asipokuwa mwangalifu, ataingia kwenye shida, kwa sababu kwa namna fulani ataelekea upande mmoja, akijaribu kulifanya rahisi, ama kupatana kidogo hapa na kidogo pale. Lakini nabii wa kweli ana amri kutoka kwa Mungu, kamwe hapaswi kupatana kwa chochote, anapaswa kabisa kuliweka papo hapo mstarini.

Hiyo ndiyo sababu Yeye alitumia roho ya Eliya sana, unaona, kwa kuwa roho hiyo daima ilitekeleza amri Zake. Mnaona? Mnaona, ilileta amri Zake jinsi hasa zilivyokuwa, na daima ni "Rudini kwenye Neno!" Mnaona? Daima inawarudisha kwenye Neno.

38 Sasa, tunauona Ninawi ukiwa katika dhambi. Basi nabii huyo alisitasita kwa sababu ulikuwa ni ulimwengu wa Mataifa, unaona, lilikuwa ni taifa la Mataifa, watu wa Mataifa; sio wake, hawakuwa ni Waebrania. Walikuwa ni Wamataifa. Merikebu kubwa, Ninawi ilikuwa ni bandari ya kibiashara, kiwanda kikubwa cha kuvua samaki kule, watu walivua samaki. Na—nao—wao walikuwa...hapana shaka walikuwa na nchi kuu iliyojaa dhambi kule. Fedha nyingi sana; na—na mahali fedha zinapatikana kwa wingi, nao watu wako kwenye maoni yanayopendwa na watu wengi wa siku hizo, dhambi daima huingia, na vurugu.

Mungu alikuwa amechoshwa nayo. Kwa hiyo Yeye alikuwa na nabii nchini, kwa hiyo akamwambia nabii Wake, "Shuka uende kule Ninawi ukapaze sauti, na kusema, 'Katika muda wa siku arobaini jiji hili litaangamizwa.'"

Sasa, Yona aliwazia sasa, "Unajua, huenda nikaingia katika shida ndogo." Kwa hiyo alitaka kuwa na hakika zaidi, kwa hiyo aliwazia atachukua likizo ndogo na—na kushuka kwenda Tarshishi. Nasi tuliona ya kwamba ninii...kulikuwako na siku arobaini tu zilizosalia. Mnaona?

Kwa hiyo Ujumbe huo ni wa haraka, wakati umekaribia. Usicheze-cheze na mambo mengine na kupata Digrii ya Kwanza na kupata kujua jambo fulani. Saa imekaribia! Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, tunajaribu kujenga shule kubwa na kuwa na mambo makubwa namna hiyo. Wakati rehema ... Jamani! Kama tukihubiri kule Kuja kwa Bwana, tuna haja gani na shule? Tunahitaji toba kwa Mungu! Mnaona?

39 Kama vile Hudson Taylor alivyomwambia yule kijana mmishenari, alisema ... Ama, kijana mvulana wa Kichina aliyemjia, akasema, "Bwana Taylor," kasema, "Bwana Yesu amenijaza na Roho Wake." Kasema, "Ni—nina furaha sana!" Kasema, "Je! nichukue miaka kumi sasa na kupata digrii zangu na kadhalika?"

Akasema, "Mwanangu, usingoje digrii. Kama mshumaa umewashwa, nenda kaitangaze! Nenda kaitangaze. Usingoje digrii. La, utakuwa umekwisha unguu nusu kabla hujazipata, digrii zako."

Hebu na, wakati unapowashwa, kama hujui jambo lingine, simulia tu jinsi ulivyowashwa. Na wala ka—kamwe usijaribu kupachukua mahali pa mtu mwingine, ama mahali pa kitu fulani. Unapojua, tangaza tu yale unayojua kwamba ni Kweli, "Hivi ndivyo lilivyonijia mimi, na hivi ndivyo nilivyojisikia juu Yake." Hiyo ni ... Kama hujui zaidi ya hayo, sema hilo! Hima twendeni! Ujumbe ni wa haraka, wakati umekaribia.

40 Sasa, vipi kama Isaya angesema, "Vema, sasa nitangojea nione jinsi anavyoendelea na jipu hilo, kwanza, mnaona. Mnaona jinsi—jinsi ninii...?"

Mnaona, Mungu alimwambia, "Nenda pale ukamwambie, sasa hivi!" Mnaona?

Naye akamwambia Yona aende. Loo, jamani!

Basi wakati alipofika huko katika bahari hiyo na bahari yenye kina, na—nayo merikebu ikakwama kwenye dhoruba, nao ikawabidi kutweka matanga na kisha kuzunguka tena na tena, walishangaa kulikuwa na shida gani kule. Bali wasingeweza kujua, ilionekana kama kitu hicho kilikuwa kikijaa maji. Na—na kila mtu akimlilia mungu wake, na muda si muda mnajua... Yona alikuwa kwenye likizo yake, kwa hiyo aliwazia afadhali hata alale, na hapana budi alikuwa ameshuka akaingia kwenye kiambaza cha merikebu

hiyo, na kulala huku ameinua miguu yake, amelala. Naye akasema, "Amka, ewe mvivu, ukamwite Mungu wako!" Naye Yona alijua shida ilikuwa ni nini.

Vivyo hivyo kila mtu anajua shida ya siku hizi! Mnaona?

41 Naye akasema, "Yote ni makosa yangu. Nichukueni mkanifunge mikono yangu, mkanitupe baharini, ndipo shida hii itaisha." Nao walionekana ni jamaa waungwana wala hawakutaka kufanya hivyo, bali wakakuta kwamba yeye alikuwa ni nabii na alijua yale aliyokuwa akisema. Akasema, "Ni—nilifikiri ningechukua likizo yangu kwanza, bali—bali Bwana hataki nichukue likizo hii. Sina budi kushuka kwenda kule, nina kazi ya kufanya. Nilifikiri ningepumzika kidogo kabla sijaenda, bali sina budi kwenda. U—ujumbe ni wa haraka, sina budi kufika kule."

Ningewazia, wakati yule samaki fulani aliyekuwa amewekwa tayari alipommeza Yona tumboni mwake, aligeuka na kurusha maji kote nchini, na kuelekea Ninawi upesi alivyoweza. Mungu alikuwa akiupeleka huo ujumbe kule katika huyo samaki aliyekuwa amewekwa tayari. Naye akaenda mbio Ninawi upesi alivyoweza, kwa kuwa a—alikuwa amembeba mjumbe na ilimbidi kumpeleka kule. Alichukua meli isiyohahi, bali Mungu alikuwa amemwandalia meli.

Kwa hiyo, mnajua, Mungu anaweza kufanya mambo makuu kama tu tutamsikiliza. Mnaona? Yeye—Yeye atafanya Yeye atafanya njia mahali pasipo na njia. Yeye Ndiye Njia. Mnaona? Na wakati Ujumbe ukiwa ni wa haraka kabisa, kama ulivyo siku hizi, Mungu huandaa njia.

42 Tunaona tena wakati Amosi ... Nilihubiri juu ya jamaa huyu, Amosi. Kama ungependa kuisoma hadithi hiyo siku moja, ni nzuri sana, isome hadithi ya Amosi, mlango wa kwanza wa Amosi. Yeye ni mfano mwingine wa ma—maonyo kabla hukumu haijaipiga dhambi. Sasa, lile jiji alilokuwa akienda kulionya, kule, lilikuwa ni kundi la Wayahudi a—ambalo kwa namna fulani wote walitoka kwenye njia ya kweli nalo lilikuwa limekuwa kituo kikuu cha watalii. Na—nami nawazia, kama nilivyotoa ule mfano asubuhi ile, nikizungumza juu yake, ya kwamba, wakati kichwa chake chenye upara kilipotokeza juu ya kilima na maskini macho yake mazee yakasinyaa wakati alipoangalia chini na kuona dhambi ya taifa hilo kuu la watu, ndevu zake nyeupe wakati akizipapasa jinsi hiyo. Jamani, ni kitu cha namna gani! Lakini hakuna mtu anayejua alikotoka.

Hakuna mtu anayejua hao manabii, wanajitokeza tu kutoka mahali fulani na kuondoka vivyo hivyo.

43 Lakini yeye aliingia mjini akiwa na "BWANA ASEMA HIVI! Tubuni, la sivyo mtaangamia! Kwa maana Mungu ataliangamiza taifa hili. Yeye ata—ataifuta mahali hapa duniani. Umefanya mapatano na adui yako. Nanyi mna—mna amani, ndivyo mnavyodhani, na adui wenu, bali wakati wote Waashuri wana—wanaongezeka kule nje. Hamwezi kutembea wawili pamoja msipokuwa mmepatana. Hivyo tu." Kwa hiyo akasema ...

Na Mungu anatutaka tujitenge. Anatutaka "tutoke ulimwenguni," sio kujaribu kuishi pamoja na ulimwengu na Mungu pia, sio kujaribu kujifananisha na ulimwengu na Mungu pia. Inakubidi kumwisha Mmoja ama huyo mwingine, huna budi kumwamini Mmoja ama huyo mwingine.

44 Na sasa tunaona ya kwamba, huyu Amosi, bila shaka alibashiri hukumu juu ya watu hawa wasipotubu. (Na—na, jamani, i—inalingana vizuri sana na siku zetu.) Nafikiri jiji hili kubwa, tukirejea kwenye hili tena, jiji hili kubwa kule chini, jinsi ambavyo lote lilikuwa limepotoka, na—na uchumi mkuu waliokuwa nao wa kila kitu, limefanikiwa. Nao walidhani walikuwa hasa katika mapenzi ya Bwana, kwa kuwa walikuwa wakifanikiwa. Lakini waligundua ya kwamba Mungu daima si mwanzilishi wa ufanisi. La, Mungu ... Wakati mwingine ufanisi unapoingia makanisani, hujitenga Naye.

45 Mnajua, Mungu alinena juu ya Israeli wakati mmoja, kasema, "Nilikupata makondeni umejaa damu, nami nikakuosha na kukuingiza ndani," apate kuwa mtoto Wake Mwenyewe. "Na ndipo ulipokuwa mkubwa, na ukawa ni msichana mrembo, ulifanya ukahaba." Akasema, "U—u—unajitoa tu kwa kila mpitaji." Mnaona? "Lakini ulipokuwa maskini na mhitaji, wakati—wakati ulipokuwa na haja, ulinitumikia. Bali nilipokubariki nawe ukapata mali nyingi, ndipo uliniacha." Na karibu imetokea kuwa hivyo. Loo, jamani!

Sasa, tunaona ya kwamba nabii huyu kweli alilishambuliwa hilo taifa, huyu Amosi. Yeye alikuwa tu ni kijana mwongoza jembe la kukokotwa na ng'ombe. Lakini tunaona ya kwamba alipofanya hivyo, alipowacharaza na kuwaambia itakavyokuwa, na kuwaambia kama hawakuwa sawa na Mungu ni kwamba adui huyo waliyekuwa wamefanya mapatano naye angekuwa ndiye hasa angewaangamiza.

46 Sasa tunaona ya kwamba Marekani yetu yenye kiburi haitaepuka hasira ya Mungu. Kama nilivyozungumza siku moja tangu nimekuwa hapa, nina hakika ilikuwa ni hapa, juu ya kila kitu katika mwisho. Mnajua, si—siwezi kuona kitu cha kujengea. Huwezi kujiundia siasa, zimekwisha. Hu—huwezi kujenga maisha ya kijamii, kwa sababu yameharibika sana. Hakuna—hakuna—hakuna kitu unachoweza kujenga huko. Wala huwezi kuweka matumaini juu ya kitu cho chote.

"Vipi kuhusu kanisa?"

Vema, huwezi kufanya chochote na kanisa, ni baridi sana na limekwisha, hakuna kilichosalia. Tayari yameuza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa mlo wa supu nzito, nayo yanaingojea tu hukumu. Roho Mtakatifu amelipitia taifa hili, akionyesha ishara Zake na maajabu, nao sikuzote wanaikataa neema Yake. Yeye anajithibitisha na kujihakikisha, kwa thibitisho Lake kuu, ya kwamba Yeye ni Neno la Mungu lililodhihirishwa katika siku hii. Nao wangali wanalikataa. Mnaona? Hakuna kitu kilichosalia sasa. Huwezi kamwe kumfanyia Mungu jambo hilo daima. Mnaona?

47 Vema, tunaona, kwanza, Yeye anawatuma manabii Wake wakiwa na onyo. Yeye habadilishi njia Yake, njia Yake ya kufanya mambo.

Sio kila mara ambapo Yeye huadhibu akiisha kuonya. Ninawatakeni mwangalie nukuu hii. Mungu hutoa onyo bali si kila mara ambapo Yeye huadhibu wakati ule ule anaponya. Mliona jambo hilo? Na halafu basi asipoadhibu akiisha kutuma onyo, basi nabii anadhihakiwa, "Hukuwa Nao. Ulisema uongo. Hu—hukusema kweli."

Jambo lile lile huenda lilisemwa—kwa Isaya. Unafikiri mtu huyo aliwazia nini wakati alipopanda kwenda kule na kutabiri ya kwamba huyo mfalme "atakufa," kisha akashuka akarudi na kusema, "La, yeye ataishi"?

48 Vipi kuhusu Yona akipitia mitaani, akisema, "Loo, jiji hili litaangamizwa katika siku kadhaa, siku arobaini," na halafu Mungu hakuliangamiza?

Mnaona, inawapasa kuangalia, sikuzote Mungu haangamizi kila anaponya. Lakini Yeye ... Kuna jambo moja, ndipo nabii huyo hudhihakiwa. Lakini kama yeye ni nabii aliyethibitishwa akiwa na Neno la Bwana, mnaona, ishara za Mungu, amethibitishwa, kama Mungu alivyosema nabii angethibitishwa (ambapo watu hawa walithibitishwa), mnaona, Neno lake silo lake, bali ni Mungu, nalo litatimia. Halina budi kutimia kama ni Neno la Mungu. Kuna kitu kimoja tu kinachoweza kulikomesha, hicho ni toba ya haraka.

49 Angalia, Amosi, yeye—yeye aliishi kuuona unabii wake, bali wakati Amosi aliponena juu ya jiji hilo, jinsi itakavyotukia, jinsi ambavyo Mungu atawafanya Waashuri waingie na kuwachukua mateka, na kadhalika namna hiyo, na jinsi ambavyo upotovu wao wenyewe ungewamaliza. Mbona, ninaamini kama ni sasa hivi... Ninaangalia hapa chini kwenye Maandiko, na kama niliihesabu hii vizuri, ni karibu miaka hamsini baada ya Amosi kutabiri. Na, sasa, mnawazia nini? Kizazi kizima kilipita kabla unabii wa Amosi haujatimia. Lakini kama mtasoma hapa, linawaambia, na yalitukia vile vile neno kwa neno yale alivyosema. Mnaona?

Yohana aliona Kitabu cha Ufunuo. Haikutukia kamwe katika siku yake. Lakini tunaliona likitimia vile vile hasa. Mnaona?

Danieli alitabiri juu ya siku ile, juu ya siku yake na kotekote. Kamwe hakuishi kuuona. Akasema, "Nenda zako, Danieli. Yeye alisema, "Nenda zako, Danieli. Kifunge kitabu—kitabu, na—na kifunge kitabu. Nawe utalala katika kura yako, lakini siku hiyo utasimama." Mnaona?

Sasa, mnaona, ninii ... sikuzote si ... Mungu...huhukumu mara anapotabiri. Unabii wa Amosi, kama nilivyosema, ulikuwa ni miaka hamsini baadaye, ulitimia. Lakini ulitimia!

50 Na halafu nabii ni—ni...wa Biblia ... Nabii halisi, wa kweli ni mtu maalum. Sio "maalum," kuwa tofauti na mtu mwingine yeyote, bali ana kazi maalum. Mnaona? Na, akiwa na agizo maalum, hana budi kuwa ni maalum (kidogo hafanani na wengine) kusudi apate kufanya jambo hilo.

Ni kama tu vile Mungu amewafananisha *manabii* Wake kuwa ni "tai."

Sasa, tai ni ndege maalum. Yeye ni ndege tu, bali yeye ni ndege maalum. Naye anaweza kuruka juu zaidi kuliko ndege wengine. Anaweza kuona mbali zaidi kuliko ndege wengine. Na, sasa, kusudi apate kwenda juu zaidi, hana budi kujengwa kusudi apate kwenda juu zaidi. Na ingemfaa nini kwenda huko isipokuwa angeweza kuona kile alichokuwa akifanya baada ya yeye kufika pale? Mnaona? Kwa hiyo hana budi kuwa ni ndege aliyeumbwa maalum. Mnaona? Kwa namna fulani yeye yuko katika—katika familia ya mwewe, yeye ni "mrarua kwa mdomo." Naye hula ninii...wengi wao ni wala mizoga. Kuna karibu aina arobaini za tai.

51 Lakini, mnaona, kanisani kuna mchungaji, na mchungaji huyo ni mtu maalum. Yeye amejengwa kufikia mahali anapoweza—anaweza kuvumilia mizozo ya watu. Yeye—yeye—yeye ni mbeba mizigo, yeye ndiye maksai wa timu. Yeye—yeye ni mtu anayeweza kuketi chini wakati ninii...mtu fulani ana neno dhidi ya mtu mwingine, na kuketi chini pamoja na hizo familia mbili (wala asichukue upande wowote) na kuhojiana na kuwapatanisha kurudi kwenye upendano. Mnaona? Yeye—yeye ni mchungaji, anajua jinsi ya kushughulikia mambo.

Mwinjilisti huyo ni mtu maalum. Yeye ni mtu anayewaka moto kama kimondo. Yeye huingia hima mjini na kuhubiri ujumbe wake, kisha anatoka huko anaelekea kwingine. Mnaona, yeye ni mtu maalum.

Mwalimu ni mtu maalum. Yeye huketi kitako chini ya upako wa Roho naye anaweza kuyachukua

Maneno na kuyaweka pamoja kwa Roho Mtakatifu, jambo ambalo, mchungaji ama mwinjilisti, yeyote wao, asingeweza kulinganishwa naye.

Halafu basi, tunaona, mtume ni mtu maalum. Yeye ni—yeye ni “mweka utaratibu.” Yeye ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu kuweka mambo katika utaratibu.

52 Nabii ni mtu maalum. Nabii ni mtu ambaye hujiliwa na Neno la Bwana, kwa sababu nabii ameumbwa hivi kwamba (maisha) dhamira yake ya ndani na dhamira yake ya kwanza ziko karibu sana hata yeye halali apate kuota ndoto yake, yeye huiona wakati akiwa macho kabisa. Mnaona? Sasa, hilo ni jambo ambalo Mungu hana budi kufanya. Mnaona, yeye anaona kinachoendelea.

Nabii huona mbali sana, mnaona, mambo yanayokuja. Anaona kikombe cha hasira ya Mungu, kimejaa, kabla hakijajazwa. Mnaona? Anaweza kusema, “BWANA ASEMA HIVI! Mungu ataliangamiza jiji hili msipotubu.” Kwa nini? Yeye ni tai. Yeye huruka huko juu sana. Mnaona? Naye anaangalia kule mbali sana na kuona kikombe hicho cha hasira kikimwagwa. Hicho ndicho nabii anaangalia. Yeye haangalii yanayoendelea hapa, anaangalia huko ng'ambo! Yeye anasema, “Inakuja!” Anaweza kwenda juu sana hata anaweza kuona kivuli hicho. Yeye alisema, “Ulimwengu utaingia giza—giza na giza kuu.” Yeye yuko juu vya kutosha, jua linawaka sasa, bali anakiona kile kivuli kikija, na yeye ana—yeye ana—yeye anasema anachoangalia. Hakijaja bado, bali hakika kitakuja! Hiyo ni kweli. Litakuja, giza kuu juu ya watu. Anajua linakuja, lingali umbali wa miaka kadhaa, hata hivyo analiona.

Amosi, yule nabii wa Mungu aliyetiwa mafuta, yeye aliona gi—giza na hukumu. Aliwaona Waashuri wakishuka kuja na magari yao kupitia kule, wakiwaua hao watu. Aliona jambo hilo likija na hukumu ya Mungu juu yao, sasa, miaka hamsini kabla halijatukia. Lakini, unaona, akiwa ni nabii, yeye aliinuliwa katika Roho na kuona jambo hilo likiwa mbali sana. Mnaona? Aliona kikombe, kimejaa, kabla hakijajazwa.

53 Kama vile Ibrahimu. Mungu alimwambia Ibrahimu, “Uzao wako utakuja kwenye nchi hii na kuwa wageni hapa kwa muda wa miaka mia nne, kisha nitawatoa kwa mkono wenye nguvu, kwa kuwa uovu wa Waamori haujatimia bado.” Mnaona? Mungu alijua kikombe hicho kitajaa. Alikuwa akinena na nabii Wake, Yeye alimwambia sasa, “Mnaona kile kikombe cha Waamori kule chini,” mnaona, “bali uovu wao haujatimia bado, Ibrahimu. Usiseme neno juu yake sasa, tulia, bali itatimia. Na wakati kikombe chao kitakapojaa, na hiyo miaka mia nne, nitawatoa kama nzige mbele zako, nami nitauimarisha uzao wako hapa katika nchi hii.” Amina! Huyu ni nabii wa Bwana.

54 Sasa, wakati anaponena juu ya ono lake, kama ni hasira ama kama ni uponyaji, huenda likakawia, bali halina budi kutimia kama ananena katika Jina la Bwana. Mnaona? Huenda ikawa ananena baraka kwako. Huenda akakwambia jambo fulani, nawe huwezi kuliona hata kidogo. Unasema, “Inawezekanaje? Mbona, ni ninii ... Mi—mi—mi ... Yeye aliniambia 'BWANA ASEMA HIVI, *Hili* litatukia, na *lile* litakuja kutukia,” wala halijatukia. Mtu huyo amekosea!” Sasa utahukumiwa kwa kutokuamini jambo Hilo, lakini litatukia hata hivyo! Mnaona? Halina budi kutukia!

“Hata likikawia,” Biblia ilisema, “hata hivyo litanena katika majira yake.” Litatimia.

55 Nabii anaangalia tu mbali na kuona kitu fulani. Yeye anazungumza juu ya kile anachoangalia. Yeye hawazii juu ya mahali hapa na vile mnavyoonekana sasa, anaangalia yale yatakayotukia. Na anaponena hayo, kama yako katika Neno la Bwana, tayari yamenenwa wala hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kuyazuia (mnaona, hiyo ni kweli,) ila Mungu Mwenyewe tu.

Angalia, sasa tunaona ya kwamba wakati ... Yeye—yeye hutamka ono lake, nabii hulitamka. Sasa, wakati mwingine yeye hunena mambo mazuri, ananena juu ya uponyaji wenu. Vema, huenda mkawazia, “Kamwe haliwezi kutimia, sijapata nafuu zaidi.” Basi hilo linafanya nini? Hilo linaleta tu hukumu za Mungu juu yako. Hiyo ni kweli. Mnaona? Yesu aliahidi kukuokoa kama ungeamini; usipoliamini, hali—halitatendeka kwako. Huna budi kulikubali, huna budi kuliamini. Mnaona? Na huna budi kujua linatoka wapi, hiyo inakupa imani yako katika Mungu; ama, nabii wako. Mnaona? Huna budi kuliamini.

56 Na sasa tunaona hapa, ya kwamba manabii hawa walionena, wa—walinena na yale waliyosema yakatimia. Na kama hasira ya Mungu imemwagwa juu ya watu, kuna jambo moja tu ... Kama nabii huyo alisema ya kwamba kitu fulani au kingine kitatukia, kuna jambo moja tu ambalo litauzuia mkono wa Mungu, hilo ni toba. Hilo ni toba kwa Mungu, ndiyo inayoizuia hasira Yake. Sasa, msilingojee, lifanye wakati huo! Mungu anaposema jambo lolote, lifanye papo hapo.

57 Hezekia, mara alipojua ... Yeye alikuwa ni mtu mzuri, bali Mungu alisema, “Wakati wako umefika, Hezekia, na—na sina budi kukuchukua. Ni—ninataka kukuchukua, nitakutwaa juu. Tengeneza mambo yote ya nyumba yako.”

Na a—a—akasema, “Itanichukua muda wa miaka kumi na mitano kufanya jambo hilo, Bwana.” Mnaona? “Sasa, ni Wewe ... Mimi—mimi—mimi ninajua ninaondoka, bali itanichukua miaka kumi na mitano kutengeneza mambo ya nyumba yangu. Siwezi kufanya hivyo sasa hivi. Si—sina wakati wa kuyatengeneza. Kamwe si—si—siwezi kuyamaliza. Bwana, jalia niishi miaka mingine kumi na mitano kusudi

nitimize jambo hili. Siwezi kuweka nyumba yangu ...”

Mnaona, agizo la Mungu lilikuwa, “Tengeneza mambo ya nyumba yako!”

Ndipo Hezekia akasema, “Siwezi kuyatengeneza mwaka huu, itanichukua muda. Nitakirejesha *hiki*, kisha nikitengeneze *hiki* na kukipeleka kwa jamaa huyu hapa, itanichukua muda wa miaka kumi na mitano kufanya hivyo. Nisamehe tu kufanya jambo hilo. Hebu ni- ... hebu ... nipe muda kidogo wa kufanya jambo hilo.” Mnaona?

Ndipo Mungu akasema, “Nita—nita—nita—nitakuwa mpole.” Lakini ilimbidi kufa hata hivyo, mnaona.

58 Na halafu tena, alichukua wakati wake, alirudi nyuma kwenye wakati huo. Mnaona? Naye angalikuwa bora zaidi kama angaliondoka bila kutengeneza mambo. Hiyo ni kweli. Lakini alimpa muda wa miaka kumi na mitano zaidi kutengeneza mambo ya nyumba yake. Kwa sababu, upesi, alifanya nini? Alisema, “Bwana, mimi ni mwenda pole. Ninahitaji miaka kumi na mitano kufanya jambo hili. Umeniagiza kutengeneza mambo ya nyumba yangu. Siwezi kufanya hivyo katika miaka kumi na mitano kwa kuwa nina mkopo hapa, na nina *hiki* huku, na nina *hiki* huku cha kufanya.”

Sasa, yeye alikuwa ni mcha Mungu, na Neno la Mungu halina budi kutimia kwa vyovyote vile. . Litatimia kwa vyovyote vile, bali Yeye alilichelewesha tu kwa kitambo kidogo, mnaona, kulizuia lisimpate. Ndipo akatenda dhambi wakati huo. Akasema, “Sitalifanya limpate yeye, bali nitalipatiliza juu ya watoto wake baada yake.” Mnajua hadithi hiyo.

59 Sasa, tunaona ya kwamba toba ya upesi wakati mwingine huizuia hasira ya Mungu kwa muda fulani.

Sasa, tunaona ya kwamba Ninawi ... Mungu alisema, “Shuka uende kule na ukapaze sauti kwenye mji huo sasa, na uwaambie, 'Kama...katika siku arobaini kitu hicho kitaanguka.'” Na, jamani, walitubu kweli! Mara walipomwona nabii huyo akipitia mtaani, akisema, “BWANA ASEMA HIVI, 'Mahali hapa pataangamia katika muda wa siku arobaini! Mahali hapa pataanguka!'” Ninii ...

Hata mfalme aliamrisha ku—ku—kufunga kote nchini, maombolezo, “Vaeni nguo za magunia, jipakeni majivu! Sio juu ya kichwa chako mwenyewe na juu ya mwili wako na juu ya nyama zako, bali juu ya ng'ombe wenu, juu ya wanyama wenu wa kondeni, jipakeni majivu na mvae nguo za magunia.” Ni toba iliyoje!

60 Sasa, tunapochunguza hapo, tunaona, kama nabii hatakuwa mwangalifu upesi sana, unaona, aweke akili zake pamoja na kumwendea Mungu, utaona kitu fulani papo hapo, kama usipokuwa mwangalifu...

Sasa mwangalie Isaya, alitoa tu unabii wake, akarudi tena ndani ya kibanda chake cha nyikani. Na, alipofanya hivyo, Bwana kamwe hakumjibu mfalme aliyekuwa akiomba. Yeye ana njia ya kufanya mambo. Kulikuwa na nabii nchini. Neno la Bwana humjia nabii Wake. Alitoka akaenda kule na kusema, “Isaya, rudi ukamwambie nimeyasikia maombi yake. Nimefahamu kwamba ni...ya kwamba anawazia itamchukua muda wa miaka kumi na mitano kufanya jambo hili. Nimeona machozi yake kwa sababu alitaka sana kufanya kazi hiyo. Itamchukua miaka kumi na mitano, alisema, kuifanya. Nenda kamwambie nitamruhusu apate hiyo, basi.” Mnaona?

Kwa nini? Yeye alimwagiza—alimwagiza Isaya kwenda kumwambia, “BWANA ASEMA HIVI!” Basi kama kuna badiliko lolote katika jambo hilo, ama kukawia... Litatukia kwa vyovyote vile; a—alikuwa hata hivyo. Lakini alisema Kama kuna jambo lolote katika hilo, basi Yeye anawajibika kurejea kwa mtu yule aliyemtumia BWANA ASEMA HIVI. Yeye alimwambia Isaya, “Rudi huko nje ukamwambie.”

61 Sasa, Yona alichukua msimamo tofauti, anapanda juu ya kilima na kusema, “Vema, afadhali hata nisingalizaliwa.” Na, loo, jinsi alivyoendelea! Na Mungu akaufanya mtango mdogo ukue na kumfanyia kivuli mpaka akapoa kule juu. Lakini akasema, “Sasa, hapa, nilishuka nikaenda kule chini, nao watasema mimi ni nabii wa uongo.”

Ndipo Mungu akanena naye, akasema, “Angalia mji huo kule chini! Angalia kule, Yona, kwamba mji mzima unatubu kwa nguo za magunia na majivu.”

Ndipo akamwambia kuhusu ule mtango mdogo na mdudu aliyeukatilia mbali. Siku moja, Bwana akipenda, ninataka kuja maskanini na kuchukua mfululizo juu ya Yona tu. Loo, kuna ninii nyingi sana kubwa...ule upepo wa mashariki ukivuma, na kadhalika. Loo, jamani! Kuna mambo mengi sana mle ndani, yanainii tu ... yanasisimua. Dhahabu hizo mle ndani, zote zinatoa mfano mle ndani, kikamilifu. Hata humleta Yesu Kristo ndani yake, na cho chote kile. Bila shaka, kila mstari katika Biblia unamleta Yesu Kristo. Naam, bwana. Hilo ndilo somo letu la Jumapili, kwa hiyo tutaona hilo, Bwana akipenda.

62 Na tazama, kuna mambo ambayo wewe ... Kama wewe ni mwaminifu na unamwambia Mungu ... Sasa, huna budi kuangalia.

Sasa nataka kuwaonesha Yona mwingine jukwaani usiku wa leo.

Usiku mmoja kulikuwa na watu waliokuja hapa. Huenda mama huyo akawa (baadhi ya watu wao) hapa usiku wa leo, kwa hiyo sitataja jina hilo, huenda labda mnajua yeye ni nani. Lakini walikuja hapa, kundi zuri la watu kutoka huko Kentucky, nao wa—walikuja hapa kwa miaka mingi. Lakini watu, wakiwa ni watu wazuri, marafiki wangu wazuri. Jamani, walikuwa—walikuwa ni marafiki wangu halisi, bali wao ... Moja tu ya namna ile ya watu ambao, wakati uamsho ulipokuwa ukiendelea wangekuja kanisani, wakati uamsho ulipokwisha, na mzigo ulikuwa ukilemea, hamna mtu angeuvuta. Na watoto wote walikuwa hapa kwenye shule ya watoto wadogo, walikuwa na ninii...tulipokuwa na madarasa yetu na kadhalika.

63 Na siku moja nilikuja nyumbani, yapata miaka minne iliyopita, ama mitano, kitu kama hicho. Naye msichana huyu mdogo, (ambaye alikuwa na umri wa karibu miaka minane wakati alipokuwa kwenye shule ya watoto wadogo), alikuwa ameolewa na alikuwa na watoto wawili. Naye alikuwa amelala hapa hospitalini, akiwa katika hatari ya kufa. Alikuwa na mimba ya karibu miezi minne, mitano; naye mtoto huyo alikuwa amekufa, wala wasingeweza kumfanyia upasuaji kwa maana alikuwa na sumu damuni. Nao wasingemfanyia upasuaji, kwa hiyo iliwabidi kumwacha mama huyo afe, pia. Hawawezi kumfanyia upasuaji, na, unaona, mtoto huyo mchanga angemuua namna hiyo, kwa hiyo iliwabidi...alikuwa tu yuafa, hivyo tu, hapakuwapo na uwezekano kwake.

Nilitoka kwenda kumwona, alikuwa ametuma nitwe. Nami nikaingia hospitalini, na huyo hapo chini ya hema ya oksijeni. Nikakiinua kifuniko hicho kidogo, nikazungumza naye kidogo, na nikasema, "Je! unanikumbuka?"

Akasema, "Hakika, Ndugu Bill, nakukumbuka."

Nikasema, "Imekuwaje ... Unaelewa jinsi ulivyo mgonjwa?"

Akasema, "Ndiyo." Kasema, "Hiyo ndiyo sababu nilituma uitwe."

Nikasema, "Vema, mbona, wewe ukoje na Bwana?"

Akasema, "Ndugu Bill, ni—nimeninii ... Si—siko tayari kwenda."

Vema, hapo tukapiga magoti na kuomba, na mama yake na mume wake, wengi wao chumbani humo, ndipo mama yake na mume wake wakaanza kulia. Na—na halafu mimi—nikamwuliza, naye akajiweka sawa na Mungu (akatimiza nadhiri zake kisha akarudi na kumwahidi Mungu; na kama angesamehewa; jinsi alivyompenda; na anazisikitikia dhambi zake, jinsi alivyokuwa ameishi), na akaendelea na toba yake na kulia. Na baada ya kitambo kidogo niliamka na kutoka nje ya jengo hilo.

64 Ndipo ke—kesho yake asubuhi wakanipigia simu, nirudi huko. Na, nikakuta, walikuja asubuhi hiyo kwa uchunguzi na kuona jinsi su—sumu ya damuni ilivyokuwa imeenea, nao wakakuta kwamba hakuwa na hata chembe moja yake. Yote ilikuwa imekwisha, kila chembe ya sumu hiyo ilikuwa imemwacha. Madaktari walikuwa wamesisimkwa sana hata wakasema, "Jamani! Mbona, hili, tunapaswa... Ni kitu cha ajabu sana." Kasema, "Tuta—tutamtayarisha," kisha kasema, "kama ingali itakuwa jinsi hiyo ifikapo asubuhi..." Kasema, "Tutaendelea kumpa penisilini," ama chochote walichokuwa wakimpa, kudhibiti maambukizi. Kasema, "Tutamfanyia upasuaji na—na kumwondoa mtoto huyo aliyekufa kabla hajaingiza kitu kingine." Kasema, "Kama yuko sawa, basi ..."

65 Vema, mara mbili ama tatu siku hiyo walimfanyia uchunguzi tena. Ndipo usiku huo, usiku sana, wakamfanyia uchunguzi, hakuna kasoro, alikuwa mzima kabisa. Ndipo wakamtayarisha. Wakamtoa kutoka chini ya kihema cha oksijeni. Kila kitu kilikuwa sawa. Walikuwa wamfanyie upasuaji kesho yake asubuhi, kumtoa yule mtoto mchanga.

Vema, nilienda huko. Na kwa sababu jambo hili lilifanywa ... Sasa, sikujua jambo hilo kamwe, sikujua kamwe. Bwana kamwe hakuniambia cho chote kuhusu jambo hilo. Ungeweza kuwauliza watu, ukitaka. Kwa hiyo wao ... yeye ... Kamwe hakusema ingekuwa hivyo. Lakini, loo, jamani, kuona jambo kama—kama hilo! Mumewe, akiwa ni mwenye dhambi, akaja na kusema, "Ndugu Branham, na—nataka kuyatoa maisha yangu kwa Bwana Yesu."

Nami nikasema, "Vema, piga magoti hapa tu na ushike mkono wa mkeo, na kisha mtembee maisha haya manyofu pamoja."

66 Mama akarudi, akasema, "Ndugu Branham, unajua, mimi hapa pamoja na watoto wangu," kasema, "sote tumekuwa tukiingia na kutoka, na tukiingia na kutoka, na karibu na Maskani, na kadhalika. Tunaketi na kukusikiliza ukihubiri, kisha tutaenda madhabahuni na kurudi." Kasema, "Nimerudi nyuma, pia, Ndugu Branham." Akasema, "Ninataka kumrudia Bwana Yesu, kwa ajili ya wema Wake kwa mtoto wangu." Vema, mnaona, hilo—hilo ni zuri sana, bali hamji kwa Bwana Yesu kwa sababu ya jambo hilo.

Karibu na usiku wa manane, saa kumi na mbili, saa moja, mama yake alilala usingizi. Naye akasema, akamwita, akasema, "Mama."

Naye akasema, "Naam, mpenzi, unataka nini?"

Akasema, "Unajua, nina furaha sana!"

Akasema, "Nina furaha sana kwa wewe kuwa na furaha."

Kasema, "Nina amani na Mungu." Kisha akasema, "Loo, ni vizuri iliyoje!"

Katika dakika chache, tena akapiga simu, akasema, "Mama."

Kasema, "Naam?"

Kasema, "Ninaenda nyumbani."

Naye akasema, "Ninajua unaenda." Akasema, "Ndiyo, kipenzi," kasema, "daktari atamtoa mtoto huyo kesho. Halafu yapata siku moja ama mbili, wakati upasuaji wako utakapopona na uondoke hapa, utarudi nyumbani na kufurahi tena, wewe pamoja na mume wako na hao watoto wadogo, na uwe Mkristo na kumwishia Mungu."

Akasema, "Mama, namaanisha ninaenda kwenye Nyumba yangu ya Mbinguni."

Akasema, "Hakika, mpenzi, mwishoni mwa safari."

Akasema, "Huu ndio mwisho wa safari." "Loo," akasema, "sasa, kuna nini?"

Kasema, "Mwisho wa safari." Kwa hiyo akasema, "Naam, mama, baada ya dakika chache nitakuwa nimeondoka."

Vema, alidhani alikuwa tu na wasiwasi na fadhaa. Akamwita nesi, huyo nesi akachukua upumuaji wake. Kila kitu kilikuwa cha kawaida. Na katika dakika tano alikuwa ameondoka, alikuwa amekufa.

Ndipo wakati niliporudi nyumbani, katika juma moja ama mawili baadaye... Nafikiri Ndugu Graham alihubiri mazishi ya msichana huyo. Niliporudi nyumbani na Meda akaniambia ya kwamba msichana huyo alikufa usiku huo, jamani, nisingeninii... Ni—nilienda kumwona mama yake. "Naam."

67 Wala si—si—sijui ni jambo gani lililonifanya nifanye hivyo, bali nilisema, "Bwana Mungu, u—unaniwia ufahamu," (Mnaona?) "Baada ya mimi kutoka kwenda kule na—na kumwambia huyo mume, naye akija kwa Bwana baada ya Wewe kumfanyia mambo haya, na yote jinsi hiyo, kisha unauchukua uhai wa msichana huyo namna hiyo." Nikasema, "Unaniwia ufahamu."

Unapomwambia Mungu kitu kama hicho, Yeye atakuacha umeketi peke yako. Sininii... Yeye simdai kitu. Nina deni Kwake. Vema, aliniacha tu nivimbishe midomo kwa siku chache, mwajua. Na, baada ya miezi mitatu ama minne, siku moja nilikuwa ukingoni mwa kijito na Bwana akasema nami katika ono, na kusema, "Sasa nenda kwa mama yake, na umwambie mama yake hivi, 'Hivi wakati wake haukuja mwaka mmoja kabla ya hapo, wakati alipokuwa akizama katika kijito, kwenye pikiniki? Alipaswa kwenda wakati huo, lakini ilinibidi kumchukua alipokuwa tayari kwenda.' Na hiyo ndiyo sababu haya yote yalitukia na ndiyo sababu ya wewe kwenda kule."

Ndipo nikaketi na kulia. Nikasema, "Bwana Yesu, nisamehe, maskini mtumishi Wako mpumbavu. Haikunipasa kamwe kusema hivyo, Bwana."

68 Nami nilikuwa nimerudi kwa mama huyo, aliishi hapa kwenye Mtaa wa Soko, nami nikamwendea, na nikasema, "Ninataka kukuuliza swali."

Akasema, "Hakika, Ndugu Bill."

Nami nikasema, "Je! Ni kweli kwamba msichana huyu alikaribia kufa maji?"

Akasema, "Hiyo ni kweli, Ndugu Branham." Kasema, "Mume wake na wao—iliwabidi kumtoa kwenye kijito." Kisha kasema, "Iliwabidi kumfanyia upumuaji bandia, na kumgandamiza, nao iliwabidi kuchukua mtambo na kumtoa hayo maji." Kasema, "Alikuwa amevaa sketi yake. Walikuwa wakifanya pikiniki. Alikuwa kule naye akakanyaga changarawe kidogo, akateleza akatumbukia kwa kichwa chake na akanyongwa majini. Hawakumwona. Kisha mara wakamwona akipanda na kuzama, nao wakakimbia ndani wakamshika na kumtoa." Kisha akasema, "Karibu afe." Kasema, "Yeye ..."

Nikasema, "Huo ulikuwa wakati wake wa kwenda."

Mnaona, Mungu anajua yale anayofanya. Sasa, Bwana labda angeniambia jambo hilo kama nisingekuwa nimechukua msimamo niliochukua, "Bwana, ninakudai, kuniambia kuhusu jambo hilo." Humdai chochote!

69 Nilisimama kwenye mkutano usiku mmoja na kumsikia mwinjilisti akimwomba mgonjwa, kasema, "Mungu, ninakuamuru umponye mtu huyu!" Ni nani anayemwamuru Mungu? Mnaona? Ha—ha—hata si ninii—si jambo la busara, unaona, kwa kuwa Mungu, Yeye—Yeye hutenda analotaka kutenda.

Je! u—udongo unaweza kumwambia mfinyanzi, “Kwa nini ukaniumba hivi?” Mnaona? La hasha! Lakini kama nabii atatulia kisha amtafute Mungu apate jibu, kuna jibu pale. Mnaona?

Ni kama tu vile mtu huyu alivyokuwa akiuliza juu ya swali la u—u—uzao wa nyoka, mnaona. . A—angalieni tu, wala m—msiwe—msiwe na haraka sana. Na halafu, sasa, Mungu daima hutimiza kila kitu kwa manufaa ya wale wampendao Bwana.

70 Sasa, kama—kama Ninawi usingalitubu, basi hukumu za Mungu zingalikuwa juu yao. Sasa kumbukeni, nabii hana budi kusikiliza. Lilikuwa ni onyo.

Sasa, jambo lile lile kwa taifa hili. Ndipo unasema, “Ndugu Branham, Jumapili iliyopita ulisema 'Hakukuwako na tumaini'?” Naam! “Kwa nini?” Liliukataa mwito wake. Halina budi kupokea hiyo. Litapokea hiyo. Kuna wakati unaokuja ambapo taifa hili litavunjika-vunjika. Niliona jambo hilo mwaka wa 1933. Mnaona, nilianguka huko mbali.

Mlisema, huenda mlisema, “Vema, halikutukia wakati huo.”

Lakini litatukia! Wala Mussolini hakuwa mamlakani, wala Ngome ya Maginot haikuwa imejengwa, wala gari halikufanana na yai katika siku hizo, na kadhalika, wala wanawake hawakumchagua Rais ambaye angeonekana kama—kama mvulana wa chuoni, na mambo haya mengine yote, wala kusingekuwako na Rais Mkatoliki, na kadhalika, aliyenenwa habari zake. Yapata miaka thelathini iliyopita, ama zaidi, mambo haya yalibashiriwa, bali Yeye alinionesha tu yangali mbali sana.

Na wakati kitu hicho kinapokaribia, wakati baada ya wakati, kikombe hicho kinaendelea kujaa! Nayo toba imehubiriwa na Billy Graham, Oral Roberts, na wengineo. Manabii, na kadhalika, wamepitia taifa hili kwa ishara na maajabu, nalo daima linagaagaa katika dhambi. Hiyo ndiyo sababu hawatubu, toba huleta jambo hilo.

71 Angalia, Ahabu kamwe hakutubu alipokemewa na Eliya. Kama Ahabu angalitubu na kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu, jambo hilo lisingalitukia. Lakini Ahabu alishuka akaja pale naye akalichukua shamba la mizabibu la Nabothi na akamfanya auawe kinyama, na mambo hayo yote maovu. Na Yezebeli ... Huyu nabii alitoka akaenda kule akiwa na BWANA ASEMA HIVI! Lakini walifanya nini? Alitishia tu kumwua. Ni kitu gani kilichotukia? Unabii wake ulitimizwa, mbwa wakamla na kuilamba damu ya Ahabu. Ni sawasawa tu kulingana na neno lake! Aliona kikombe, kimejaa.

Hiyo ndiyo sababu maskini yule Mikaya, akisema jambo hili hili, angeweza kubariki kile Mungu alichokuwa amelaani? Mnaona, neno la—lake, unabii wake, ulipatana na Neno.

72 Herode, kamwe hakutubu wakati Yohana aliposema, “Si halali kwako kumchukua huyo, mke wa ndugu yako!” Yeye hakutubu kamwe. Lakini alifanya nini? Mkewe alihitaji kichwa cha nabii. Angalieni uchafu uliompata. Angalia kilichompata. Angalia, hata leo, huko Uswisi, ya—yale maji ya bluu ya kumkataa yangali yanachemka kama—kama kumbukumbu. Mnaona, hakika, yeye hakutubu wakati alipokemewa na Bwana. Yohana alimwambia, haidhuru yeye alikuwa ni nani (liwali, ama chochote alichokuwa; ama mfalme mkuu, ama yeyote yule), hana budi kutubu Mungu anapoita, la sivyo hasira iko juu yake!

Ni mara ngapi katika manabii... Nimeyaandika hapa chini, bali hatutakuwa na wakati kwa kuwa nina kama dakika kumi zilizosalia.

73 Kama hakuna toba, basi hukumu hakika itakuja! Hezekia alitubu. Mnaona? Ninawi ilitubu.

Ahabu hakutubu kamwe. Nebukadreza hakutubu kamwe. Watu katika siku za Nuhu hawakutubu kamwe, na hukumu iliingia moja kwa moja. Mnaona? Sasa, lakini Yeye kwanza humwonya kila mtu. Kila mtu hupata onyo.

Sasa, tukiona wakati umekaribia, hebu kila mtu anayejisikia ya kwamba kuna onyo, atubu upesi kabla hasira ya Mungu haijashuka.

Sasa hebu na tulishushe kwenye Maskani ya Branham. Mnaona, tumeyaona mambo haya na tunajua kwamba ni ya Kweli. Tunajua ya kwamba ni Kweli kabisa. Agizo la Neno ni, “Kama mtatubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, mtaapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa watoto wenu na hao walio mbali.” Mnaona?

74 Sasa, mtu fulani, Bw. Dauch, aliniuliza hapa si muda mrefu uliopita, yeye alisema, “Ndugu Branham, ninazeeka. Ninadhofika, tisini na moja.” Akasema, “Je! Unadhani—mimi niko tayari kufa? Unafikiri niko tayari kwenda? Je! unafikiri nimeokoka?”

Nikasema, “Bw. Dauch, je! uliwahi kwenda kwa da—daktari kwa ajili ya kupimwa afya ya mwili wako?”

Akasema, “Naam.”

“Nawe unamwambia ... Sasa, kile daktari anachofanya, ana kitabu kilichowekwa pale, naye

hukichukua kitabu hiki na kuchunguza. 'Sasa, jambo la kwanza ninalipaswa kumfanyia mtu huyo, ni kuchunguza moyo wake.' Kwa hiyo anachukua stethoskopu na kuziweka maskioni mwake, anauchunguza moyo wake." Kisha nikasema, "Halafu, kitu kingine anachochukua, yeye huangalia presha yake ya damu, kwa—kwa presha mkononi mwake. Halafu kitu kingine anachofanya, anachukua sampuli ya mkojo, na chochote kile zaidi, na damu kidogo kutoka kwake, na mambo haya yote mbalimbali. Yeye hupitia yote, na kama hawezi kupata cho chote ... Anachukua eksirei. Kama hawezi kupata kitu, angesema, 'Bw. Dauch, wewe ni—wewe ni mzima kimwili.'

"Yeye anaweka msingi huo juu ya nini? "Yeye anaweka msingi huo juu ya nini? Juu ya hali kutoka kwenye kitabu chake cha matibabu, kwamba kama kuna kasoro yoyote kulingana na mwanasayansi mkuu kitaonekana hapa, kitafanya *hivi* hapa, kitafanya *vile* pale. Hivyo basi, kadiri anavyoweza kujua lolote kuhusu jambo hilo, wewe ni mzima, mnaona, kimwili.

75 "Sasa," nikasema, "katika jambo hili, ni—ninalipa uchunguzi wa nafsi. Mnaona? Na Mungu, kwa ajili ya nafsi, ana chombo kimoja tu, hiyo ni kweli, hilo ni Neno Lake. Hilo ni Neno Lake. Na Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:24, 'Yeye alisikiaye Neno Langu.' Sasa, *kusikia* huko hakumaanishi kusikiliza tu kelele. Hilo *sikia* linamaanisha 'kulipokea.' 'Yeye anayeweza kulipokea Neno Langu,' amina, 'yeye alisikiaye!' ' (Usisimame kimya, uliite upuuzi, 'Mambo hayo, hakuna lolote. Siliamini Hilo.') 'Yeye asikiaye Neno Langu!' A-ha. Hilo ni Neno la Yesu, ambalo, Yeye ni Neno. Haya basi. 'Kama unaweza kulisikia Neno Langu,' Yeye alisema, 'na kumwamini Yeye aliyenipeleka, amepita kutoka mautini kuingia Uzimani; wala hata hataingia Hukumuni, bali tayari ameipita.' Amina!" Nikasema, "Moyo wako unadunda vipi sasa?"

Akasema, "Ninaliamini. Nimelisikia. Nimelipokea."

Nikasema, "Basi kulingana na Mtaalamu Mkuu, Mpasuaji Mkuu, Daktari Mkuu wa Uzima wa Milele anasema, 'Umepita kutoka mautini kuingia Uzimani wala kamwe hutaingia hukumuni.'"

76 Kasema, "Nilipokusikia ukihubiri juu ya Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ubatizo wa maji, nilienda moja kwa moja nyuma yako nawe ukanibatiza." Kasema, "Mimi ... Mtu niliyekuwa wakati mmoja, mimi si mtu huyo tena. Jambo fulani limetukia kwangu. Sikuwa nikilijali kitu na nilienda kwingine, bali nimegeuka na kuanza kwenda huku. Na moyo wangu unawaka mchana na usiku kumkaribia Yeye. Kila Neno Lake, ninaliamini! Ninasema, 'Amina!' kwa kila sehemu Yake. Sijali linanikataje, ninataka kujipima moja kwa moja na Hilo. Nami nimefanya hivyo kadiri nijuavyo mimi."

Nikasema, "Kwangu mimi inaonekana kana kwamba moyo wako unapiga vizuri sana. Ni—ninaamini ya kwamba u—u mzima kiroho sasa."

Akasema, "Sijui kama ingekuwa wakati Unyakuo utakapokuja, je! ninaweza kuingia katika huo, Ndugu Branham?"

Nikasema, "Si mimi kusema ni nani anayeingia ama ni nani asiyeingia."

Akasema, "Vema, ningetaka kuwa hai, ni—ninatamani sana kuuona Unyakuo."

77 Nikasema, "Vema, hebu nione yale Ki—Kitabu cha Sayansi kinayosema hapa, juu yake, na sayansi ya nafsi hapa." . " Nikasema, "Vema, Kinasema hivi, katika Wathesalonike wa Pili, mlango wa 5, Kilisema, 'Sisi tulio hai na tuliosalia hata Kuja kwa Bwana hatutawazua' (hilo linamaanisha 'kukawilisha') 'hao wanaostarehe, waliolala. Kwa maana parapanda ya Mungu italia, na hao waliolala ama wanaostarehe wataamka kwanza, wavae kutokupatikana na mauti. Kisha sisi tulio hai kwenye siku hiyo, wakati huo hao wakiisha kufufuka, mnaona, ndipo tutabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua, na kukutana nao; ndipo tutapaa juu kumlaki Bwana hewani, tutanyakuliwa pamoja nao.' Kama ukilala, kama hulali, kama utalala ama hutalala; popote utakapozikwa, hata kama hutazikwa kabisa, unakuja haidhuru! Hakuna kitu kinachoweza kukushikilia. Utakuwako kule!" Nikasema, "Ndugu Dauch, kama Yesu hatakuja mpaka vitukuu vya vitukuu vya vitukuu vya vitukuu vyangu, ungali utakuwa pale moja kwa moja kwenye wakati hasa, nawe utakuwa pale kabla hata hawajabadilishwa, kama wakienda." Hiyo ni kweli. Amina!

78 Kunakuja baraka kama vile tu hasira inavyokuja. Loo, hatuna budi kuwa tukitafuta moja ya hayo usiku wa leo. Huna budi kuwa ukiitazamia hasira ikuangukie na maangamizi, au huna budi kuwa ukiutazamia ufufuo wa Bwana Yesu. Mungu yeye yule aliyeahidi moja, aliahi-... Nina furaha sana!

Ninatazamia kuja kwa ile siku ya Utawala wa Miaka Eflu,
Wakati Bwana wetu mwenye rehema atakapokuja kumchukua Bibi-arusi Wake
anayengoja;

Loo! moyo wangu una shauku sana na tamaa ya kule kuwekwa huru kutamu,
Hapo Yesu wetu atakaporudi duniani tena.
Ndipo dhambi na huzuni, uchungu na mauti ya ulimwengu huu wenye giza yatakoma,
Katika ule utawala wa fahari pamoja na Yesu wa miaka elfu moja ya amani; (Loo,
jamani! "Nasi tutakuwa pamoja na Bwana milele." Mnaona?)

79 Yale Mungu aliyosema, hayana budi kutimia. "Nao watajenga nyumba, watakaa ndani yake.

Watapanda mizabibu, nao watakula matunda yake. Hawatapanda akaichukua mtu mwingine. Watapanda mizabibu yao na kukaa nayo." Amina! Amina! "Hawatadhuru wala kuharibu katika Mlima Wangu wote mtakatifu." Haleluya!

Wakati huu wa kufa utakapovaa kutokufa, mauti ha—haya yatakapomezwa katika ushindi, ndipo tutamwona kama alivyo na kuwa na mwili kama Mwili Wake wenye utukufu. Loo, ni wakati wa ulioje ujao!

80 Mungu yeye yule na manabii wale wale waliolibashiri Neno la Mungu, ama hasira itakayomwagwa, kumwagwa, pia walinena juu ya baraka hizi zijazo. Nina furaha sana! Mungu kamwe ha—haliletei taifa ma—maangamizi bila ya kulionya. Hamletei mtu maangamizi bila ya kumwonya. Na sasa kama Yeye hufanya hivyo, tuna jambo fulani ambalo limetupata, thibitisho la ishara za siku za mwisho ziko pamoja nasi, yule Roho Mtakatifu mkuu akitenda kazi miongoni mwetu na kulitia kanisa moto kwa Uwepo Wake, akilithibitisha Neno Lake. Basi kanisa linajiandaa kwa ajili ya kupaa hewani moja ya siku hizi, kwa nguvu za Mungu. Kwa kuwa ni onyo la kuweka kando kila mzigo na dhambi ituzingayo kwa upesi, kusudi tupige mbio sana kwa saburi katika mashindano haya yaliyowekwa mbele yetu, kwa Mwenye Kuanzisha na Mwenye Kutimiza Imani yetu.

81 Mungu awabariki, enyi kanisa! Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika! Naam, bwana. Kama ukisikia Uwepo Wake, mwendee. Kama kuna jambo lolote baya moyoni mwako, lisahihishe. Hatuna wakati mwingi uliosalia, Kuja kwa Bwana kumekaribia. Unamwamini? Loo, jamani! Si kutakuwa ni kuzuri kule? Ni wakati wa jinsi gani, nitakapowaona mashujaa wa kale huko nyuma wakitembea kupitia kwenye ile Paradiso! Loo, jamani! Ninautazamia wakati huo.

82 Ninakumbuka nikimsikia ndugu yangu akisema, wakati akirudi kutoka nchi za ng'ambo, kutoka kwenye vile viwanja vya vita na kadhalika, kasema, "Maskini mashujaa hao, walipoiona ile Sanamu ya Uhuru, na kuwavingirisha walemavu wao wapate kuiona ile Sanamu ya Uhuru." Hiyo ndiyo unayoiona kwanza, ukiwa melini, unapokaribia, kwa sababu ni ndefu sana. "Na kuuona ule mkono, umesimama kule," kasema, "hao watu huzirai tu na kulia. Na hao watu wakubwa tu wanasimama pale, wanaanguka tu kwenye sitaha wanaanza kulia." Ilikuwa ni kitu gani? Ishara ya uhuru. Kila kitu walichowahi kupenda kilikuwa papo hapo nyuma ya ishara hiyo hapo.

Loo, lakini itakuwaje wakati nitakapoisikia ile meli ya kale ya Sayuni ikipiga king'ora asubuhi hiyo na nione bendera zikipepea! Hapo vita vitakapokwisha na ushindi umepatikana, haleluya! Nasi tunakuja Nyumbani, ambapo mauti, dhambi na kuzimu zimeshindwa; wala hakuna dhambi tena, hamna mauti tena, hamna huzuni tena. Ninaweza tu kusikia filimbi ikipigwa! Loo, tunaukaribia ule Mji. Naam, bwana. Mawimbi yanaingia, ile meli ya kale inaelekea mahali pake. Mungu, tusaidie kuishi kwa ajili ya saa hiyo!

83 Bwana Yesu, sisi ni watu ambao tuna—tunajaribu tuwezavyo, kwa yote yaliyo ndani yetu, kutembea katika Nuru ya injili ya Injili Yako kuu ambayo uliifia upate kuiweka sawa. Tunashukuru sana kuona, katika siku hizi ovyo zenye giza tunazoishi sasa katika saa hii, kwamba tunaona ishara zikitokea. Ee Mungu, kwa kuwa ni maandiko ya mkono kwenye ukuta, tunakushukuru, Bwana, ya kwamba tunaweza kuyaona na kujua ya kwamba ukombozi umekaribia. Tunahubiri, tunaenda nchini kote, tunakuona Wewe ukifanya ishara kuu, ukijionyesha kila siku, kila mwaka. Hakuna mwaka unaopita pasipo ishara Yake (kuu) ya Kimbinguni kuipiga dunia. Nasi tunaona jambo hilo, tukijua ya kwamba jeshi kuu la Mungu linasonga mbele.

Loo, si wengi kwa idadi, bali ni kundi lenye nguvu jinsi gani lililo na Uzima wa Milele! Kasema, "Watakimbia kupitia katikati ya jeshi na kuruka ukuta." Naam, "jeshi" la mauti halitakuwa na vizuizi kwake, Yeye atalishinda. Ataruka "ukuta" kati ya mambo ya kawaida na ya Kimbinguni, na kwenda moja kwa moja mikononi mwa Mungu, kuingia katika ule Umilele mkuu. Bwana Mungu, tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili. Tunajua wakati umekaribia.

84 Ninaomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo kama kuna wengine hapa wasiokujua Wewe, ambao hawajafanya amani yao ... Na labda usiku wa leo, wakati tumekuwa tukizungumza, Sauti ndogo imekuwa ikizungumza ndani ya moyo wao, "Ninasikia onyo kwamba siwezi kuwa huku muda mrefu zaidi." Ee Mungu, jalia watengeneze mambo ya nyumba yao, sasa hivi. Jalia kila kitu kiwekwe vizuri. Jalia ubaridi Labda wao ni Wakristo, bali hawajaninii tu ... Wameishi chini ya jambo hili muda mrefu sana na kuona mambo mengi sana, wame—wamepoteza tu thamani Yake. Ni ... Mambo hayo, wanayachukua kwa wepesi badala ya kulichukua kwa kilindi cha moyo na unyenyekevu sana.

Ee Mungu, jalia tujichunguze usiku wa leo, tujalie, tukijua ya kwamba mambo haya makuu yanatuonya tu juu ya Kanisa kunyakuliwa hivi karibuni. Na endapo tumelemewa na dhambi, na kutokuamini, na uzembe, hatutafaulu huo unyakuo. Tunajua jambo hilo, Bwana, kwa hiyo tunaomba ya kwamba Wewe utamwasha moto Roho Mtakatifu ndani yetu, ndani ya mioyo yetu. Ee Mungu, ziwashe moto nafsi zetu kwa baraka Zako. Tusaidie kuelewa.

85 Sasa, wabariki watu pamoja. Mbariki mchungaji wetu wa thamani na mkewe. Wabariki mashemasi, wadhamini, washiriki wote, pamoja. Tusamehe dhambi zetu. Yaponye magonjwa yetu, Bwana. Na

kuiwasha moto mioyo yetu. Na jalia tutoke mahali hapa tukiwa na ujumbe wa maonyo, tunapokutana na watu walio katika dhambi, na kuwaambia, "Ewe rafiki, hivi huoni aibu kwamba unafanya mambo kama haya, ukijua ya kwamba huna budi kukutana na Mungu siku moja?" Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, sasa; naukabidhi Ujumbe huu, na yote pamoja, kufanya kazi pamoja kwa ajili ya utukufu Wako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

86 Hivi hamumpendi? Wazieni kile tulicho. Angalieni umbali tuliosafiri barabarani, enyi marafiki. Angalieni tu huko nyuma barabarani kutoka huko mbali, katika siku za Luther na Wesley, kote katika nyakati. Angalieni hapa mahali tulipo: papa hapa penye kilele cha piramidi; papa hapa ambapo Mungu amelithibitisha, kwamba Biblia kupitia ile mihuri saba imefunuliwa kikamilifu; tukiingojea tu zile siri saba moja kwa moja pale mwisho, kwenye kule Kuja kwa Bwana na Kunyakuliwa kwa Kanisa ambako kunaweza kutukia kabla ya asubuhi. Loo, jamani!

Nampenda, (kwa uaminifu sasa) nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

87 Tukiwa kwa ukimya sasa... Je! mnatambua ya kwamba kila mmoja wetu humu ndani hana budi kuondoka hapa, kuondoka humu ulimwenguni? Je! mnajua ya kwamba mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake ni chache nazo zimejaa taabu? Mlijua ya kwamba kwa sababu tulizaliwa kwa mti huo kutoka kwenye Bustani ya Edeni, wa mauti, ya kwamba hatuna budi kufa? Sisi ni tunda la tumbo la uzazi la mama yetu, nasi hatuna budi kufa, hatuna budi kutengana na maisha haya. Vijana ama wazee, haileti tofauti yoyote. Kama mwanamume ama mwanamke aliye na umri mkubwa sana aliye humu ndani akiishi usiku huu, huyo mume ama mke ataishi zaidi ya watoto wengi wenye umri wa miaka kumi, kumi na mitano? Mamia ya hao watakufa kote ulimwenguni kabla ya mapambazuko, mamia ya watoto. Kwa hiyo cha muhimu tu, ni, unafanya nini sasa hivi?

88 Huenda hii ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho. Vijana au wazee, mnaweza kwenda kanisani. Usiache jambo moja bila kufanywa. Maanisha kabisa na uwe mwaminifu sana. Weka kila dhambi na kila kitu kando. Angalia moja kwa moja mbele za Mungu na uulize swali, "Bwana, ninakupendeza? Ningefanya nini kingine, Bwana Yesu? Kamwe sitakuwa na nafasi tena, baada ya maisha haya kwisha, kukutumikia Wewe. Huu ndio wakati pekee nilionao. Bwana Mungu, nijalie tu ni nini unachotaka kufanya! Kama ningenda kufanya jambo *hili* au ningefanya *lile*, ningefanya kwa furaha."

Je! Sisi—je! Tunafikiri hivyo kwa uaminifu? Je! vijana wanawazia hivyo? Je, watu wa makamu wanafikiri hivyo? Je, wazee wanafikiri hivyo? Matineja wanawazia hivyo? Hatuna budi kwenda, na mnajua kwamba sisi sote hatutakuwa tumeondoka kabla ya mapambazuko? Hatujui. Unasema, "Hilo linanitia wasiwasi." Halikupasi! Kwa kweli, linapaswa kukupa furaha kuu kujua ya kwamba unaondoka kwenye maskini nyumba hii ya kale ya wadudu.

89 Kuna ulimwengu mwingine. Sio lazima uende mbali sana. Uko papo hapo pamoja nawe. Umekuzunguka. Wewe tu...wewe... Mungu alikupa tu hisi tano, na hizo ni za kuwasiliana zaidi sana na huu, ulimwengu huu. Bali kuna ulimwengu mwingine ambao huna hisi zozote za kuwasiliana nao, huwezi kuwasiliana nao kwa sababu hunazo.

Kwa mfano, nilisema, Jumapili usiku, (labda hamkulipata) vile...tuna hisi tano: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Lakini vipi kama usingalikuwa na kuona (ulikuwa tu na kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia), na mtu mwingine alipokea kuona kwao na kusema, "Kuna ulimwengu mwingine, jua"? Hizo—hizo hisia, unajigonga kwenye vitu, na kile kitu hicho kilicho kinaweza kukwambia kwamba ni kitu gani. Mbona, ungefikiri mtu huyo alikuwa na kichaa, maana huna hiyo—hiyo hisi ya—ya kuona. Hakuna mtu aliyepata kuwa nayo, umjuaye. Umewasikia watu waliosema mambo kama hayo, bali uliyatilia shaka. Lakini tunajua kwa hisi hii kwamba ni halisi. Ni mahali halisi. Mnaona? Ni—ni—ni—ni mahali ambapo ... unaweza kuona. Hisi yako inatangaza jambo hilo.

90 Sasa, jambo pekee unalofanya unapokufa, unabadilisha tu hizo hisi tano (Utukufu! Whiu! , unapokea tu hisi nyingine. Nawe uko hai ukiwa na hisi bora zaidi, bora zaidi mara maelfu kuliko hii, katika maisha mengine; maisha ambapo hakuna mauti, ambapo hapana huzuni. Na mambo ambayo hujui kitu juu yake sasa, unayaona dhahiri unapovuka kule. Huyaelewi sasa kwa sababu unajigonga-gonga kwenye hayo, huna hisi hiyo. Unasema, "Ni—ninasikia hisi ya kigeni hapa usiku wa leo. Inaonekana kwangu kama kuna ... Ninataka tu kulia, au kupaza sauti, ama kitu fulani." Ni Malaika wa Bwana. Mnaona?

91 Kama vile mtu fulani anasema, unajua, ambaye kamwe hakuwa na hisi ya kuona, aseme, "Mara kwa mara ninahisi kitu kilicho halisi, nasikia kitu kama joto."

Unasema, "Ni nuru ya jua."

"Nuru ya jua ni nini? Sikuwahi kuiona." "Hakuna ninii..." Mnaona, kamwe hajapata kuiona, hajui ni nini. Mnaona, inambidi mtu fulani hapo amwambie, mtu anayeweza kuiona. Loo, jamani! Mnaona?

Tunabadilika tu. Tunabadilika tu, msilogope mauti. Mauti si kitu ila ni sanamu ya kutishia. Yesu aliishinda. Hata wakati Paulo alipofika mwisho, yeye alisema, "Mauti, u wapi uchungu wako? Li wapi tishio lako? Kaburi, ku wapi kushinda kwako? Unasema umenipata? Mimi—mimi ninataka kukuelekeza kule nyuma Yerusalemu. Liko kaburi lililo tupu kule na 'Mimi Ndimi niliyekushinda wewe, mauti na kuzimu pia,' nami nimo ndani Yake wala huwezi kunishikilia! Nitafufuka tena." Loo, jamani! Yeye alisema, "Nimewekewa taji, ambayo Bwana, Hakim mwenye haki, atanipa mimi; wala si mimi tu, bali na wote wanaopenda kufunuliwa Kwake."

92 Unampenda. Mnataka kumwona akija. Mnamngojea. Ni hadithi ndefu, ni—ni kungojea kwa muda mrefu. Ni swala la upendo. Bali kamwe huwezi kungojea mpaka utakapomwona! Loo, jamani! Hivyo ndivyo ilivyo. Loo, huo ndio wakati tunaotazamia, huo ndio wakati! Iwapo moyo wako hauko jinsi hi—hi—hiyo usiku wa leo, rafiki, kuwa mwangalifu. Mnaona? Kuwa mwangalifu. Usiache adui akudanganye. Wakati Roho Mtakatifu humu ndani anapotaka kuruka kwenda kwa Muumba Wake, kwa Bwana Wake, kuna swala la upendo ambalo hakuna mtu anayeweza kusimulia habari zake. Hiyo ni kweli, ni halisi. Ni halisi.

Kwa hiyo kama kuna onyo, linalosema, "Huko tayari kwa ajili ya jambo hilo," basi kumbuka, Mungu huenda anakutayarisha kwa ajili ya jambo fulani. Mnaona? Huko tayari...

93 Unasema, "Vema, kama nikibatizwa, Roho Mtakatifu, basi, vema, labda Mungu atanichukua?" La, si hilo tu, ndio tu unajiandaa kuishi. Hu—huko tayari kuishi mpaka utakapompata Roho Mtakatifu, na kisha unapompata Roho Mtakatifu basi uko tayari tu kuishi. Hukuwa tayari kuishi kabla ya hapo, mnaona, bali sasa uko tayari kuishi baada ya kumpata Roho Mtakatifu. Mnaona? Kukuandaa tu. Mnaona?

Watu husema, "Vema, sina budi kujiandaa kufa." Loo, jamani, ninajiandaa kuishi! Amina. Jambo lenyewe ni kwamba, jiandae kuishi, ishi katika Kristo! Maisha ya ushindi juu ya dhambi, mauti, kuzimu, tayari nina ushindi. Yeye ndiye Ushindi wangu nami ndiye ushahidi Wake, nami ni ushuhuda wa Ushindi Wake. Amina! Hivyo ndivyo ilivyo.

94 "Unajua je unaye?" Ninaye. Amina. Yeye alinipa Huyo kwa neema Yake. Ninamsikia. Ninamjua. Ninamwona akitenda kazi maishani mwangu. Alinibadilisha. Na kulingana na Kitabu hiki hapa, Yeye alisema ya kwamba nilikuwa na Uzima wa Milele wala sitaweza kuja Hukumuni, bali nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani kwa kuwa Yeye aliniondolea hukumu yangu. Na kama Yeye alilipa gharama, usijaribu kunileta kwenye Hukumu yoyote. Yeye tayari ameniondolea, nami nikakubali hilo. Naam, bwana.

Kwa hiyo hakuna hukumu tena. Hakuna mauti tena—hakuna tena. Loo, itanibidi kuliacha kanisa na kuwaacha watu siku moja, bali hilo...Yesu akikawia. Na kama jambo hilo likitukia, mbona, jamani, mimi sijafa. Siwezi kufa, nina Uzima wa Milele. Unawezaje kufa ukiwa na Uzima wa Milele? Mnaona? Daima katika Uwepo wa Mungu na milele tutakuwa pamoja Naye! Amina! Hilo linaufurahisha moyo wangu, jamani, linanifanya nitake kuanza kuhubiri tena. Mnaona? Hiyo ni kweli. Loo, Yeye ni wa Ajabu!

Yeye si ni wa ajabu, ajabu, ajabu?

Yesu si Bwana wangu si ni wa ajabu?

Macho yameona, masikio yamesikia, yale yaliyoandikwa katika Neno la Mungu;

Yesu Bwana wangu si ni wa ajabu?

Ninaupenda ushuhuda huo.

Macho yameona, masikio yamesikia, yale yaliyorekodiwa katika Neno la Mungu;

Yesu Bwana wetu si ni wa ajabu?

95 Loo, nampenda! Yeye ni Amani yangu, Uzima wangu, Tumaini la—langu, Mfalme wangu, Mungu wangu, Mwokozi wangu, nanii wangu ... (Loo, jamani!) Baba yangu, Mama yangu, Dada yangu, Ndugu yangu, Rafiki yangu, ni kila kitu kwangu! Mnaona? Tulikuwa tukiimba wimbo mfupi kama huo. Mnajua, je! ninyi nyote mnazipata hizo nyimbo fupi za Kipentekoste kama... Natumaini wamezima kinasa sauti hicho, mnaona. Wimbo huo tuliozoea kuuimba:

Yeye ni baba yangu, mama yangu, dada yangu na ndugu yangu,

Yeye ni kila kitu kwangu.

Yeye ni kila kitu, Yeye ni kila kitu kwangu;

Yeye ni kila kitu, Yeye ni kila kitu kwangu;

Kwa kuwa Yeye ni baba yangu, mama yangu, dada yangu na ndugu yangu,

Yeye ni kila kitu kwangu.

Mnakumbuka wakati tulipokuwa tukiimba huo? Yeyote wenu anaukumbuka? Jamani, miaka mingi iliyopita! Na ndipo tulikuwa tukisema:

Ninajua ilikuwa Damu, najua ilikuwa Damu,

Ninajua ilikuwa Damu kwangu;
Siku moja nilipotea, akufa Msalabani,
Najua ilikuwa Damu kwangu.

Mnaukumbuka huo wimbo mfupi? Hebu tuone, ule mwingine tuliouimba ulikuwa ni upi? Hebu tuone.
Loo, hivi hamtatesha pamoja nami saa moja,
Ninapoenda huko ng'ambo, ninapoenda huko?
Loo, hivi hutatesha pamoja nami saa moja,
Wakati ninapoenda huko na kuomba?
Ninashinda, ninashinda,
Ninashinda, ninashinda;
Kwa maana nampenda Yesu, Yeye ni Mwokozi wangu,
Naye anatabasamu na ananipenda pia.

96 Kulikuwako na maskini mzee Ndugu Smith, ndugu mweusi, alikuwa hapa chini pembeni. Loo! Ningewasikia hao jamaa weusi huko chini, ningeketi tu pale na kupiga mayowe na kulia na chochote kile, nikalitikisa gari langu kotekote na kuruka-ruka huku na huko namna hiyo. Wote walipiga makofi. [Ndugu Branham anapiga makofi huku akiimba — Mh.].

Loo, hivi hutatesha pamoja na ...

Ule mdundo mdogo walio nao hao watu weusi, mnajua. Hakuna mtu anayeweza kuimba kama wao; afadhali usahau jambo hilo. Mnaona

... Saa moja,
Ninapoenda kule, ...

Loo, jamani! Niliketi pale, nikasema, "Ee Mungu!" Maskini mvulana huyu, mwenye umri wa karibu miaka ishirini, ningekimbia na kuzunguka na kuzunguka hilo gari na kupaza sauti tu na kumsifu Mungu namna hiyo. Loo, ni wakati ulioje! Hiyo ilikuwa ni siku za mwanzoni tu, wakati Mungu alipokuwa akitenda kazi miongoni mwa watu jinsi hiyo. Sasa tunakuwa Kanisa lenye nguvu. Si wafuasi wengi, bali lenye nguvu katika Roho. Amina. Ni ajabu iliyoje!

97 Halafu kulikuwa na wimbo mfupi... Ninakumbuka siku ile huko chini Chattanooga, Tennessee, wakati nilipokutana na huyu... Sio Chattanooga, ilikuwa ni kule chini Memphis, mahali nilipokutana na maskini mwanamke huyu mweusi, mnajua, akisimama pale. Mmenisikia nikisimulia habari zake, mnajua. Mvulana wake alikuwa na ugonjwa wa zinaa. Naye alikuwa na shati hili la mwanamume limezungushiwa kichwani mwake, ameegemea kwenye benchi namna *hiyo*. Naye Bwana akaisimamisha hiyo ndege pale wala asingeiruhusu kuondoka, kwa namna fulani, nao wakaniambia nije nichukue... Naye Roho Mtakatifu akasema, "Fanya matembezi mafupi ushuke uende *hivi*."

Nami nikatembea kule chini, nikiimba. Nikawazia, "Jamani, ndege yangu iko karibu kuondoka!"

Akaendelea tu kusema, "Endelea mbele. Endelea na safari. Endelea na safari." Siku za mwanzoni tu za huduma yangu.

98 Nami nikaangalia, akiegemea uani pale, na maskini kibanda kidogo, mahali padogo pale. Kulikuwako na dada mzee amesimama pale. Loo, yeye alikuwa ... Alifanana na mmoja wa hawa dada kwenye hizi chapati za Shangazi Jemima. Mashavu makubwa mno manene, mnajua, na nywele za—zake, shati lake limerudishwa nyuma. Aliegemea langoni namna hiyo, nami ninaninii tu... Nilikuwa nikiuimba ule wimbo mfupi kuhusu...mfupi... Unaitwa nini... Ninasahau jina la wimbo huo mfupi niliouimba. Sasa, ni kitu fulani kuhusu—kuhusu ... Ulikuwa ni wimbo mfupi wa Kipentekoste, yubile ndogo.

Ndipo nikaacha tu kuimba, nikafika karibu sana. Ndipo nikapitia pale. Naye alikuwa amesimama pale na machozi yakitiririka chini ya hayo mashavu makubwa manene; nilitaka kumkumbatia. Akasema, "Habari za asubuhi, mchungaji!"

Nikasema, "Shangazi, ati ulisema nini?"

Akasema, "Nilisema, 'Habari za asubuhi, mchungaji.'"

Nikasema, "Ulijuaje nilikuwa mchungaji?" Sasa, kwa watu wa Kusini, hilo linamaanisha "mhudumu," mnajua. Kasema, "Sasa, ulijuaje mimi nilikuwa mchungaji?"

Akasema, "Nilijua unakuja."

Nikasema, "Ulijua ninakuja?" Nikawazia, "A-ha, hili hapa, mnaona."

Akasema, "Naam, bwana." Kasema, "Je! u—uliwahi kusoma hadithi katika Biblia, mchungaji, juu ya yule mwanamke Mshunami?"

Nikasema, "Naam, shangazi, nimesoma."

Akasema, "Mii nilikuwa mwanamke wa namna hiyo." Akasema, "Nami nilimwomba Bwana anipe mtoto, mimi na mume wangu, nami ningemlea kwa ajili Yake." Kasema, "Alinipa, Yeye alinipa mtoto mchanga." Kisha kasema, "Nilimlea, mvulana mzuri." Kasema, "Aliambatana na kundi baya, mchungaji. Akapata ugonjwa mbaya," kisha kasema, "amelala huko ndani anakufa. Amekuwa mahututi kwa muda wa karibu siku mbili sasa. Hata hajazinduka kwa muda wa siku mbili. Daktari alikuwa hapa na akasema, 'Hawezi kuishi,' kasema, 'anakufa.' Ulikuwa ni ugonjwa wa zinaa." Kisha akasema—akasema, "Ilikuwa ni vigumu kumwona mtoto wangu mchanga akifa, nami nikaomba usiku kucha." Kisha kasema, "Nikasema, 'Bwana,' kasema, "mii nilikuwa mwanamke anayefanana na yule mwanamke Mshunami, lakini' kasema, 'yuko wapi Elisha Wako?'"

99 Ndipo kasema, "Niliingia usingizini nami nikaota ndoto, ya kwamba nilikuwa nimesimama hapa kwenye lango hili, nami nikakuona ukishuka ukija mtaani ukiwa na kofia hiyo ndogo kwa namna fulani imeinama upande mmoja wa kichwa chako." Lakini kasema, "Kuna jambo moja tu," kasema, "liko wapi lile..." Kasema, "Ulipaswa kuwa na kasha ndogo mkononi mwako."

Nikasema, "Nimeliacha tu kule chini katika Hoteli ya Peabody."

Kasema, "Nilijua kwamba ulipaswa kuwa na kasha la mkononi." Kisha kasema, "Mtoto wangu mchanga anakufa."

Nikasema, "Jina langu ni Branham."

Akasema, "Nina furaha kukutana nawe, Parson Branham."

Nikasema, "Ninawaombea wagonjwa. Umewahi kusikia huduma yangu?"

Kasema, "La, siamini nilipata kuisikia." Kasema, "Waweza kuingia ndani?" Basi nikaingia.

Jamaa huyo mkubwa akilala pale namna hiyo. Nilikuwa nikijaribu kumwambia juu ya uponyaji wa Kiungu, bali hilo silo lililokuwa likimvutia. Alitaka kumsikia mvulana huyo akisema alikuwa "ameokoka na tayari kuondoka." Naye anasema ... Naye Mungu akamwoko.

Na yapata mwaka mmoja baadaye nilimwona huko nje kama mbeba mzigo kule chini kwenye stesheni ya reli. Jinsi ambavyo Bwana hufanya mambo!

Ndipo wakati niliporudi, baada ya hapo, nilipaswa...ndege hiyo ilipaswa kuondoka saa moja, na ilikuwa ni karibu saa tatu na nusu. Basi nikachukua teksu nikarudi. Na mara nilipoingia, ikatangazwa, "Wito wa mwisho kwa safari ya ndege namba *ninii*." Bwana aliishikilia ndege hiyo uwanjani pale wakati nilipoenda na kumwomba mvulana huyo. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo.

100 Nilikuwa nikijaribu kuwazia juu ya huo, wimbo mdogo, "*Mmoja Wao*." Hivyo ndivyo ilivyo. Loo, jinsi tulivyokuwa tukiufanya huo uvume humu ndani, na kupiga makofi yetu. Tungesema:

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao; (Haleluya!)
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.
Walikuwa wamekusanyika kwenye chumba cha juu,
Wote wakiomba katika Jina Lake,
Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu, Na nguvu za utumishi zikaja;
Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo
Atawafanyia ninyi yale yale,
Ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.
Mmoja wao, mmoja wao,
Ninafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao. (Nawe je?)

101 Sikilizeni kifungu hiki.

Ingawa watu hawa huenda wasiwe wameelimika,
Au kujivunia sifa za kiulimwengu,
Wote wameipokea Pentekoste yao,
Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
Nao wanatangaza sasa, kwa mbali na kwa mapana,
Nguvu Zake ni zile zile tu,
Nami ninafurahi kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.
Loo, mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Ninafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, loo, mimi ni mmoja wao,
Ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Loo, njoo, ndugu yangu, itafute baraka hii
 Ambayo itausafisha moyo wako mbali na dhambi,
 Itaanzisha kulia kwa kengele za shangwe
 Na zitaiwasha nafsi yako moto;
 Loo, linawaka moto sasa moyoni mwangu,
 Loo, utukufu kwa Jina Lake,
 Nami ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao. (Je! Mnafurahia jambo hilo?)
 Mmoja wao, mmoja wao,
 Nafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
 Loo, mmoja wao, mmoja wao,
 Ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

102 Loo, hivi hamna furaha? Hebu na tupeane mikono mmoja kwa mwingine tunapouimba. Mnasemaje? Hebu na tufanye hivyo.

Mmoja wao, mmoja wao,
 Nafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;

Mimi nina furaha sana pia, ndugu.

Loo, mmoja wao, mmoja wao,
 Ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.
 Loo, njoo, ndugu yangu, itafute baraka hii
 Itokayo ... nafsi yako moto,
 Itakayozifanya kengele za shangwe zianze kulia
 Na zitaipasha nafsi yako moto;
 Loo, inawaka moto sasa ndani ya moyoni wangu,
 Loo, utukufu kwa ninii Yake ...

Hebu na tuinue mikono yetu juu.

Nafurahi kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Sote pamoja.

Mmoja wao, mmoja wao,
 Nafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
 Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
 Ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

103 Sikilizeni kwa makini tena sasa, mnaona.

Ingawa watu hawa huenda—huenda wasielimike kuwa, (kamwe hawakutoka chuoni)
 Au kujivunia sifa za kiulimwengu,
 Wote wamepokea Baraka yao ya Pentekoste,
 Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
 Nao wanatangaza sasa, kwa mbali na mapana, (kila kificho na pembe)
 Nguvu Zake zingali ni zile zile,
 Ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Loo, uimbeni, enyi kanisa

... wao, mmoja wao,
 Nafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
 Loo, mmoja wao, mmoja wao,
 Ninafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wa ...

Chukua lesu yako ndogo sasa.

Mmoja wao, mmoja wao,
 Nafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
 Loo, mmoja wao, mmoja wao,
 Nami ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Bwana asifiwe! Amina! Sisi ni kama watoto tu. Hatuna kitu cha utaratibu uliozoeleka kwetu. Mungu hana desturi. Hiyo ni kweli? Naam, bwana!

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
 Nafurahi sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
 Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
 Loo, ninafurahi sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wa ...

104 Je! wewe kweli una furaha unaweza kusema jambo hilo? Inua tu mkono wako, useme, "Bwana asifiwe!" [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe!" — Mh.] Bwana asifiwe! Nina furaha kwamba mimi ni mmoja wao! Nina furaha kuwa.

Bwana Mungu, nina furaha sana. Mmoja wao! Mmoja wao! Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao. Ewe Mungu, tusaide kuwa hivyo. kudumisha Nuru ikiwaka, Bwana, tunapotembea kiaskari kuelekea Sayuni. Tujalie hilo, Baba. Katika Jina la Yesu, tunayatoa maisha yetu Kwako kwa ajili ya utumishi. Amina. Amina.

Loo, tunaelekea Sayuni,
Loo, Sayuni mzuri, mzuri;
Tunaelekea Sayuni,
Ule mji mzuri wa Mungu.
Njoni, sisi tunaompendao Bwana,
Na tuzitangaze shangwe zetu,
Jiunge na wimbo kwa moyo mmoja mtamu,
Jiunge na wimbo kwa moyo mmoja mtamu,
Na hivyo mkizunguke kiti cha enzi
Na ... (Loo, imbeni tu katika Roho! ... Kiti cha enzi.
Loo, tunaelekea Sayuni,
Ule Sayuni mzuri, mzuri;
Tunaelekea Sayuni,
Ule mji mzuri wa Mungu.
Loo, tunaelekea Sayuni,
Sayuni mzuri, mzuri;
Tunaelekea Sayuni,
Ule mji mzuri wa Mungu.
Hebu wale wakataao kuimba
Wasiomjua Mungu wetu kamwe;
Bali watoto wa Mfalme wa mbinguni,
Bali watoto wa Mfalme wa mbinguni,
Wanaweza wakatangaza furaha yao kotekote,
Wanaweza wakatangaza furaha yao kotekote.

Hebu na tuuimbe huo!
Tunaelekea Sayuni,
Loo, Sayuni mzuri, mzuri;
Tunaelekea Sayuni,
Ule mji mzuri wa Mungu.

105 Loo, hilo haliwasugui kabisa? Hivi hamzipendi hizo nyimbo za kale? Ni—ni bora niwe nazo kuliko zote unazoweza ... ama zozote za aina hizi nyingine za nyimbo mnazoweza kuwa nazo. Hizo ni nyimbo nzuri, za kale za moyoni. Loo, jamani! Ninajisikia vizuri sana na mwenye furaha ninapozimba, ni nzuri tu! Jamani, ninajisikia tu kama kushangilia!

Chukua Jina la Yesu pamoja nawe,
Mtoto wa huzuni na mateso;
Litakupa furaha na faraja,
Loo, lichukue, kila uendako.
Jina la thamani (Jina la thamani!), Ee ni zuri iliyoje! (Ee ni zuri iliyoje!)
Tumaini la dunia na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Lo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la dunia na furaha ya Mbinguni.

Tukisujudu sasa:
Tukiinama mbele ya Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvalisha taji,
Wakati safari yetu ikishakamilika.
Jina la thamani, Lo ni tamu iliyoje!
Tumaini la dunia na ...

[Ndugu Neville anaifunga ibada — Mh.]



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7